# Nipashe

Jumatano Septemba 23, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580347

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710



KINAMAMA MPOO...

siasa

Nipashe · HABARI BORA NA KAMILIFU

THOMAS ISIDORE NOEL SANKARA

Tanzania ilipojibu tuhuma za UN haki za binadamu

■ Lawama za 2015 zimepotea, zaibuliwa nyingine

UKURASA 11

## Magufuli, Lissu wazidi kuchuana, madini, biashara kushawishi kura

UKURASA 2

# Uamuzi mgumu

**HATIMA** ya CHADEMA, ACT-Wazalendo kuungana mkono urais kujulikana siku chache zijazo, vigogo wajifungia kutoa msimamo... *Endelea ukurasa 3*



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, akihutubia wananchi wa Itigi, Wilaya ya Manyoni mkoani Singida jana, baada ya kumaliza mikutano ya kampeni katika Mkoa wa Tabora. **PICHA: IKULU**

## SUGU, DK. TULIA 'JINO KWA JINO' UBUNGE MBEYA MJINI

UKURASA 4



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwapungia mkono wafuasi wa chama hicho, baada ya kuwasili katika uwanja wa Kayanga, Wilaya ya Karagwe, mkoani kagera jana, kwa ajili ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MWINYI ATANGAZIA NEEMA WAJANE

UKURASA 17

**MICHEZO** SIMBA YAILETA AL AHLY KUKIPIGA KWA MKAPA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6


Fursa kwa Wagombea! 2020

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote walioptishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

# JPM atoa hadhari sera za vyama

**Na Gwamaka Alipipi, SINGIDA**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewataka Watanzania kuvipuuza vyama vya siasa vyenye lengo la kutaka kuyaweka madini dhamana kwa wawekezaji, pindi vitakapopewa ridhaa ya kuongoza nchi.

Amesema kuna baadhi ya vyama vya siasa kwenye ilani zake za uchaguzi vimebainisha mkakati wa kuweka dhamana rasilimali za nchi, yakiwamo madini, akionya kuwa kwa kufanya hivyo ni kuliingiza taifa kwenye utumwa.

Amesema wananchi wanapaswa kuvikataa kwa kutovipigia kura siku ya uchaguzi mkuu kwa kuwa vina malengo ya kuuza nchi.

Alitoa tahadhari hiyo jana akiwa katika Tarafa ya Itigi mkoani Singida, alipowahutubia wananchi na wanachama wa CCM, waliojitokeza katika Uwanja wa Polisi Square kumsikiliza akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena kuongoza nchi.

"Nimesoma kwenye ilani yao, wanazungumza kuwa wakipata madaraka, madini yetu watayaweka dhamana. Maana yake hayo madini atatafutwa mtu wa kutoka nje, anakabidhiwa madini yote anaanza kuchimba, eti ndiyo dhamana ya wao kuongoza nchi.

"Kasomeni kwenye ilani yao, yaani uchukue madini yote halafu uwakabidhi watu fulani ndiyo dhamana ya kuongoza nchi? Eti ndiyo dhamana ya kujenga barabara hii? Tunaingia kwenye utumwa," alisema.

Dk. Magufuli alisema Ilani ya CCM kuhusu rasilimali za nchi inaeleza kuwa mali yoyote itakayokusanywa hata kama ni madini itakuwa ni ya Watanzania wote.

"Madini yatakayopatikana, tutayauza kwa bei ya wakati huo, ndiyo maana tuliwabana wale wengine hadi tukaingia kwenye mazungumzo kwamba faida itakayopatikana kwenye madini tutagawana nusu kwa nusu," alisema Dk. Magufuli.

Aliongeza kuwa serikali imeruhusu kila Mtanzania wa kawaida kuchimba madini, kufungua masoko ya kununua madini aina ya dhahabu nchi nzima, madini ya Tanzanite kuzungushiwa ukuta, lengo likiwa ni kulinda rasilimali hiyo kuibiwa na wajanja.

Dk. Magufuli alisema: "Ndiyo maana leo kina Saniniu Laizer wamekuwa mabilionea. Hilo ndiyo lengo letu la kuifanya Tanzania kuwa tajiri. Sasa hao wanaopanga kuyaweka dhamana, leo wataweka dhamana kwenye madini, kesho yake wataweka dhamani kwenye wanyama wetu na mbuga zetu. Tunaingia kwenye utumwa mwingine."

Katika kampeni zake hizo, Dk. Magufuli aliwaahidi wakazi wa Tarafa ya Itigi na Mkoa wa Singida kuwatatulia kero zinazowakabili ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya afya, kupata gari la kubeba wagonjwa. Mgombea huyo pia aliwaahidi kuwajengea shule ya sekondari katika Kata za Kitaraka, Kilangali na Itigi Majengo, kujenga maabara ya sayansi katika shule za sekondari, akibainisha kuwa ni shule moja tu kati ya 11 zenye maabara katika tarafa hiyo.

Dk. Magufuli aliwaahidi wakazi hao kuwatatulia kero ya uhaba wa watumishi wa afya na kutekeleza ujenzi wa barabara kutoka Itigi- Makongorosi, Chunya kwa kiwango cha lami.




Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Reginald Munisi, akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu rufani zilizotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ( NEC ), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Lissu: Mikoa ya mipakani maalum kwa biashara

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameahidi kuigeuza mikoa iliyopo mipakani kuwa maeneo maalum kwa ajili ya uchumi na biashara.

Alitoa ahadi hiyo jana akiwa Kayanga, wilayani Karagwe, mkoani Kagera akiendelea na kampeni ya uchaguzi mkuu na kueleza kuwa, lengo ni kuruhusu wakulima kuuza mazao yao ya biashara nchi zenye bei kubwa ya zao husika.

"Mfano kama bei kubwa ya kahawa ipo Dar es Salaam tutakufanyia utaratibu wa kuuza, kama AMCOS, vyama vya msingi vinataka kununua kahawa yako lazima washindane na wanunuzi wengine ili bei iwe kubwa," alisema.

Alisema kwa sababu Tanzania ni sehemu ya soko la pamoja la Afrika Mashariki, mikoa ya mipakani inayolima mazao ya biashara itakuwa ni ya maalum ya shughuli za kiuchumi.

Vilevile, alisema Karagwe ni wakulima wakubwa wa kahawa, lakini soko lake limeanguka ikilinganishwa miaka iliyopita.

Alisema anguko hilo linasababishwa na vyama vya ushirika na mkulima akilima, akiweka kwenye gunia anaambiwa hawezi kuuza mpaka chama cha ushirika ambacho badala ya kutoa fedha kinawapa karatasi.

"Mnakopwa kahawa yenu halafu wakija kulipa wanawakata, utaratibu wa kukopa wakulima kahawa umewafanya kuwa maskini," alisema.

Pia alisema wakulima wa korosho nao wamekuwa wakifanyiwa hivyo na hiyo inasababishwa na utaratibu wa kuuza mazao vyama vya ushirika.

Hata hivyo, mkutano huo wa kampeni ulilazimika kuahirishwa kwa muda baada ya mvua kunyesha.

***Romana Mallya, Frank Maxmillian, TUDARCo na Lilian Lugakingira***

# RC akerwa na vurugu mikutano uchaguzi

**Na Mary Mosha, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameeleza masikitiko yake kuhusiana na matukio ya uvunjifu wa amani yaliyojitokeza katika majimbo ya Vunjo, Hai, Moshi na Rombo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, watu wawili wanaodaiwa kuwa makada wa Chama cha NCCR-Mageuzi katika Jimbo la Vunjo, waliokotwa katika eneo la Ghona, wakiwa wametelekezwa huku mmoja wao akiwa amekatwa sikio na mwingine kujeruhiwa vibaya na watu wasiojulikana.

Jana, Dk. Mghwira wakati anazungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uchaguzi katika majimbo tisa ya Mkoa wa Kilimanjaro, alisema mpaka sasa watu kadhaa wanashikiliwa na Polisi.

"Nchi yetu iko katika kampeni za uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu. Mpaka sasa vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki vinaendelea na kampeni kwa kuzingatia ratiba kama zilivyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), lakini kumekuwa na matukio ya uvunjifu wa amani," alisema. Alisema kumekuwa na matukio ya watu kupigwa na kujeruliwa, kutekwa, kupotezwa na kutupwa kwenye maeneo mbalimbali ya mashamba, mito na madaraja, wapigakura kunyweshwa pombe kupita kiasi kwa malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwadhuru na kutafuta taarifa.

Mkuu huyo wa mkoa alisema pamoja na kuwapo kwa matukio ya kupigwa na kutekwa, pia kumekuwapo na matukio ya wanachama wa chama kimoja kuingilia mikutano ya ndani ya chama kingine.

Kwa mujibu wa Mghwira, mambo kama hayo husababisha wanachama kupigana na hata kuumizana.

"Kufuatia (kutokana na) matukio hao yasiyoendana na maadili ya uchaguzi, watu kadhaa wamekamatwa na wanalisaidia Jeshi la Polisi katika uchunguzi sambamba na kufungua majalada. Uchunguzi ukikamilika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wote watakaobainika kuhusika na matukio hayo," alisema.

"Ili kuhimarisha hatua hizi ofsi ya mkuu wa mkoa kilimanjaro kwa kushirikiana na taasisi za dini tumeandaa kongamano la siku moja litakalohusisha viongozi wa vyama vyote, wagombea wao wa ubunge na udiwani kutoka majimbo yote tisa na timu zao za kamapeni ikiwa ni pamoja na wakuu wa wilaya na wakurugenzi kongamano hili linatarajiwa kufanyika Septemba 29, mwaka huu, "alisema Dk. Mgwhira. Aidha mwenyekiti huo aliwaagiza wakuu wa wilaya kuhakikisha vikundi vyote vyenye dalili ya uvunjifu wa amani vinadhibitiwa , na mikutano yote ya wagombea wa ngazi mbalimbali inapewa ulinzi wa kutosha .

"Ninapenda kusisitiza kuwa vurugu za namna hii si asili ya Tanzania na kwa vyovyote vile si asili ya watu wa Kilimanjaro. Kuna chuki inapandikizwa na mgawanyiko katika kuhakikisha mkoa unakuwa katika hali ya taaruki muda wote, nimekataa hilo.

"Ninawaomba sana viongozi wote wa vyama, viongozi wote wa kampeni na wagombea na viongozi wa umma na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wagombea wote wapate nafasi ya kujinadi na wananchi wapate kusikia ili kufanya maamuzi (uamuzi) sahihi siku ya uchaguzi," alisema. Aliwataka wananchi wenye mapenzi mema kutoa taarifa ili kukemea vitendo vya kikatili kwa jamii. Pia alipongeza Jeshi la Polisi kwa juhudi kubwa ilizoweka katika kusimamia amani katika maeneo yete.

Baada ya tukio hilo, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha NCCR Mageuzi, James Mbatia ambaye ni mgombea ubunge wa Jimbo la Vunjo, alieleza alivyowakuta makada wawili wa chama hicho walivyoshambuliwa na kujeruhiwa na watu wasiojulikana.

Mbatia alieleza namna alivyowakuta katika eneo la Ghona makada wake wawili Deo Mosha akiwa hana sikio na Yolanda Lyimo akiwa ameteswa.

Juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Mwandamizi (SSP) Dotto Mdoe, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba tayari polisi wameanza uchunguzi.

## HABARI KITAIFA



Mwanasheria wa Chama cha ACT-Wazalendo, Omar Said Shaaban, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu malalamiko yao kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na wasimamizi wa uchaguzi kutokana na kuenguliwa kwa wagombea wao 11 wa nafasi ya ubunge na udiwani Zanzibar. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uamuzi mgumu ACT, CHADEMA kuungana

**Romana Mallya na Evelineema Ernest (SJMC)**

HATIMA ya Chama cha ACT-Wazalendo kumuunga mkono mgombea urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, itajulikana Oktoba 3 mwaka huu.

Wakati hatima hiyo ikisubiriwa, ACT-Wazalendo imesisitiza kuwa ushirikiano wa vyama makini bado uko palepale na ndani ya muda mfupi wataeleza ni kwa namna gani utatekelezwa.

Juzi, Mwenyekiti wa chama hicho na mgombea urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, alipokuwa akihutubia visiwani huko, alisema: "Ninajua muungano, Rais atakuwa Tundu Lissu, ni rahisi kumwambia nirejeshee watu wangu, lakini hata kwa bahati mbaya apite Magufuli, nitapanda ndege kwenda Ikulu kumwambia ninataka watu wangu."

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwanasheria Mkuu wa ACT-Wazalendo, Wakili Omar Shaban, alisema ushirikiano una maslahi mapana ndani ya chama na wananchi kwa ujumla.

Wakili Shaban aliyasema hayo baada ya kuulizwa hatua zilizofikiwa na chama kuhusu mazungumzo yao ya ushirikiano na CHADEMA.

"Hatujaacha kuzungumza kushirikiana na vyama makini vya siasa, mpaka dakika hii hatujaacha kuzungumza namna gani tutashirikiana, ninawaaahidi kwamba ndani ya muda mfupi mtaitwa kuelezwa," alisema.

Alisema kama jambo hilo lipo, basi mamlaka husika ndani ya chama kwa wakati sahihi italitolea taarifa rasmi, lakini kwa siku ya jana alisisitiza kujikita kwenye masuala ya rufani na mapingamizi.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe kupitia ukurasa wake rasmi wa mtandao wa kijamii wa Twitter alisema: "Kumtoa Magufuli (Rais John Magufuli) kunahitaji maamuzi magumu na ya kishujaa kutoka kwa viongozi wa vyama vya upinzani. Bila ya kuunganisha nguvu, hatoki."

Zitto pia alisema amezunguka nchi nzima na kuona hisia za Watanzania, akidai kuna mwanamke alimfuata na kumhoji imekuwaje wameshindwa kukubaliana kusimamisha mgombea mmoja.

"Nilipata uchungu sana, Watanzania wanataka mabadiliko tunawapa," alisema Zitto ambaye jana jioni aliiambia BBC kuwa uamuzi rasmi utatangazwa Oktoba 3 mwaka huu.

Katika mkutano wake wa jana, Wakili Shaban alikanusha madai yanayoeleza kuwa kuna mgogoro wa viongozi ndani ya chama hicho unaomhusu mgombea wao wa urais, Bernard Membe.

Kuhusu mapingamizi na rufani, alidai chama kimebaini kuwapo kwa hujuma zilizofanywa na baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi dhidi ya wagombea wao walioenguliwa kwenye mchakato wa uchaguzi huo.

Alisema tayari ACT-Wazalendo imeshamwandikia barua Mwenyekiti wa NEC kuhusu suala hilo na kumwomba kupitiwa upya uamuzi huo wa kuwaengua wagombea wao hao badala ya chama kufungua shauri la uchaguzi hapo baadaye.

# Msajili awaonya wagombea lugha za matusi

**Na Betrina Bishubo, SJMC**

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, amewataka wagombea wa vyama vya siasa kuhakikisha kampeni zao hazivunji sheria kwa kusema uongo dhidi ya chama au mgombea mwingine.

Nyahoza aliyasema hayo jana katika mahojiano na chombo kimoja cha habari na kueleza kuwa matumizi ya uongo yanaweza kusababisha madhara makubwa kwa chama kinachoongelewa vibaya.

"Kunapotokea uchochezi au matumizi ya maneno ya uongo au matusi, Msajili wa Vyama huchukua jukumu la kukemea vitendo vya aina hii pale wanapokuwa na uhakika wa kutendeka kwa vitendo hivyo," alisema.

Pia alisema Msajili ana jukumu la kutoa onyo na adhabu kwa chama au mgombea endapo kutakuwa na ukiukaji wa aina yoyote wa sheria.

"Kwa kutenda kosa hilo pia kuna ulipaji wa faini kati ya Sh. milioni 10 na Sh. Milioni 50 na kukisimamisha chama kufanya shughuli za siasa kwa muda uliopangwa. Endapo mgombea atashinda uchaguzi ikiwa bado amesimamishwa atalazimika kusubiri muda ufike ndipo aendelee na majukumu yake ya kiofisi," alisema.

Pia Nyahoza aliwakumbusha wanasiasa kufanya siasa kwa kistaarabu kwa kuzingatia sheria za vyama vya siasa na kufuata taratibu za usajili ili kulinda kanuni zote za uchaguzi.


## UBALOZI WA SWITZERLAND (SA), EUROPIAN UNION DELEGATION NA HTT INFRACO LIMITED DAR ES SALAAM

### MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Switzeland (Swiss Agency), Europian Union na HTT Infraco limited watauza kwa mnada wa hadhara Magari tarehe 26 September, 2020 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Magari yatakayouzwa;**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser Hard Top | 1HZ Diesel Engine | 2011 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota L/Cruiser Prado S/Wagon | TA-VZJ120W Diesel Engine | 2004 | Haujalipwa |
| 2 | Toyota Hilux Double cabin | 2KD Diesel Engine | 2012/ 2005 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Hilux P/ UP Single Cabin | 3 L Diesel Engine | 2005 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Rav4 Station Wagon | 1AZ Diesel Engine | 2002 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Almera Saloon | Petrol Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Nissan P/up Hard Body Single cabin | QD32 Diesel Engine | 2013 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Terrano Station Wagon | Diesel engine | 2003 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Serena Min Bus | DBA-C25 Petrol engine | 2009 | Umelipwa |
| 1 | Mitsubishi Min Bus | 2.5 Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Coaster 16 Seaters | M-RB20 Petrol Engine | 1988 | Umelipwa |

Magari yote yanaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza, Lion Street kuanzia tarehe 23 September, mpaka 25 September 2020,saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 1 October, 2020 saa 10:00 jioni, ukishindwa kulipa kwa muda huo gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB bank na NBC yanakubalika.
3. Magari yote yatauzwa kama yalivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Magari yote yatakayouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

***Kwa maelezo zaidi waone:***

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**DAR ES SALAAM**

11591302


# Wajeruhiwa msikitini kwa mapanga Pemba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WATU watatu wamejeruhiwa kwa mapanga Kisiwani Pemba wakiwa katika msikiti alfajiri ya kuamkia jana wakisali.

Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, amesema katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu sio vizuri mtu kuchukua sheria mkononi kwani inaweza kuleta uvunjivu wa amani ndani ya nchi.

Aliyasema hayo katika Hospitali ya Vitongoji baada ya kuwatembelea na kuwafariji majeruhi hao ambao walicharangwa mapanga eneo la Kangagani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema, mtu yoyote haruhusiwi kuchukua sheria mikononi kwa kuwa Serikali na vyombo vya usalama vipo macho na vinaendelea kufanya ulinzi katika maeneo yote ya nchi.

Alieleza kuwa msako mkali utaendelea na yoyote ambae atashiriki kwa njia moja ama nyengine kuharibu amani na utulivu, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Daktari wa dhamana katika hospitali ya Vitongoji, Sharif Hamad Khatib, alisema, jana alfajiri wamewapokea majeruhi watatu kutoka kijiji cha Kangagani ambao baada ya uchunguzi wa madaktari walibainika wameshambuliwa kwa kitu chenye ncha kali.

Aliwataja, majeruhi hao ni Khamis Nyange Makazi Prof Gogo (65), alipata jeraha kubwa katika sehemu ya shingo, Bakar Ali Hassan (55), mwenyekiti wa maskani ya CCM Kangagani alipata jeraha katika mkono wa kulia na Kombo Hamad Yussuf (73), Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Wete alipata jeraha katika bega la kulia.

Alieleza wanaendelea vyema na madaktari wanaendelea kuwafanyia uchunguzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alisema Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi wa tukio hilo na hakuna mtu ambae alikamatwa hadi jana.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akimvalisha kofia kada wa CCM, Mzee Adam (80), mkazi wa Kyela, baada ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Uwanja wa Mwakangale, wilayani Kyela, mkoani Mbeya jana. **PICHA: OMR**

# Mbinu zakoleza moto mchuano wa Sugu, Dk. Tulia Mbeya Mjini

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JIMBO la Mbeya Mjini ni miongoni mwa majimbo kadhaa nchini, ambayo uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu unatajwa kuwa utakuwa wa ushindani mkubwa kutokana na aina ya wagombea waliosimamishwa na vyama mbalimbali.

Kwa mujibu wa Msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo hilo, Elias Ng'wanidako, wagombea wanaowania jimbo hilo ni watano ambao ni Dk. Tulia Ackson (CCM), Joseph Mbilinyi 'Sugu' (CHADEMA), Protas Mgimbila (CHAUMA), Mwakaje Kaili (NCCR-Mageuzi) na Raphael Ngode (CUF).

Hata hivyo mchuano unatajwa kuwa utakuwa mkali zaidi kati ya Dk. Tulia na Sugu, ambao bunge lililopita walikuwa wote bungeni kupitia njia tofauti.

Dk. Tulia ambaye alikuwa Naibu Spika, aliingia kupitia nafasi 10 za kuteuliwa na rais, huku Sugu akiwa mbunge wa kuchaguliwa na alikuwa anaongoza Jimbo la Mbeya Mjini kwa awamu ya pili na sasa anaisaka awamu ya tatu.

Mchuano unatarajiwa kuwa mkali kati ya wagombea hao wawili kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukubwa wa vyama wanavyoviwakilisha ambavyo ndivyo vinavyochuana zaidi hata kwenye nafasi ya urais.

Pamoja na mchuano kuwa mkali, lakini kuna vitu ambavyo wanawaahidi wananchi na vinatarajiwa kumpa ushindi mmoja wapo ikiwamo ahadi ya kutatua changamoto za wananchi.

**AHADI ZAO**

Dk. Tulia na Sugu wamekuwa wakichuana kwa kuwaahidi wananchi neema mbalimbali ikiwamo kuboresha huduma za kijamii kama maji, elimu, afya na iundombinu.

Kwa kiasi kukubwa wanasiasa hao wamekuwa wakiahidi ahadi ambazo zinafanana kwa sababu wote walikuwamo kwenye bunge lililopita na wanaonekana kuzifahamu kero za wananchi.

**MBINU WANAZOZITUMIA**

Akizindua kampeni zake Septemba 9, mwaka huu, Dk. Tulia alitumia sauti alizorekodiwa kwenye vikao mbalimbali vya bunge la 11, alipokuwa akiwaombea wananchi huduma mbalimbali za kijamii kushawishi achaguliwe.

Katika sauti hizo alisikika akiwaombea wananchi wa kata za Uyole, Iwambi, Itende, Mwansekwa na Nsoho huduma ya maji, huku pia yakisikika majibu ya Naibu Waziri, Juma Aweso, alipokuwa anatoa majibu ya ombi hilo.

Vilevile kwenye sauti hizo alisikika akimuomba Waziri wa Nishati kuwasaidia baadhi ya wananchi wa kata za Jiji hilo ambazo zipo pembezoni ziunganishiwe umeme kupitia mradi wa umeme vijijini (REA) na pia akasikika Waziri Dk. Medard Kalemani akikubali ombi hilo.

Dk. Tulia amekuwa akiwaaminisha wananchi hao kuwa endapo watamchagua, atahakikisha anaendelea kuwapigania ili waendelee kupatiwa huduma hizo na Serikali.

"Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilisikia kero zenu kupitia mimi na imetekeleza kwa kiasi kikubwa na tunaomba mtuchague ili tuendelee kuwahudumia," alisema Dk. Tulia.

Kwa upande wa Sugu amekuwa akiwaeleza wananchi kuwa katika kipindi chote alichokuwa mbunge, amekuwa akiwapigania ili wapate huduma za kijamii.

Akiwa katika Kata ya Nzovwe hivi karibuni, alisema yeye ndiye aliyesimama kwenye mkutano wa Rais Magufuli Mei mwaka jana na kuomba mradi wa maji wa Mto Kiwira utekelezwe haraka ili kuwaondolea wananchi kero.

Alisema mradi huo ndio utakuwa suluhisho la tatizo la huduma ya maji kwenye jiji hilo kuanzia jijini humo mpaka Mji wa Tunduma mkoani Songwe, na kwamba mradi huo haugharimu fedha nyingi.

"Nilimweleza rais Magufuli kuwa mradi huo ni muhimu sana, wataalamu walisema unagharimu Sh. bilioni 70 sasa kama anaweza kununua ndege kwa zaidi ya Sh. bilioni 200 hawezi kushindwa kutoa fedha za mradi huo," alisema Sugu. Vilevile Sugu amekuwa akiwaaminisha wananchi kuwa yeye ndiye aliyekuwa anawaombea huduma ya umeme, na kwamba huduma hiyo imesambaa kwa kiasi kikubwa.

Pia wagombea hao wamekuwa wakijinadi kuwa katika miaka mitano iliyopita walisaidia kuboresha huduma za afya, elimu na miundombinu ya barabara, huku wakiomba kuchaguliwa ili waendelee kuboresha.

**KUBEBWA NA WAGOMBEA URAIS**

Pamoja na Dk. Tulia na Sugu kuonekana wana nguvu ya ushawishi, lakini mchuano wao unatarajiwa kuchagizwa pia na nguvu za wagombea urais wa vyama vyao, ambao pia wanachuana kwa nguvu.

**VIJEMBE**

Wagombea hao wamekuwa wakifanya siasa za vijembe kwa kila mmoja kusema vitu ambavyo vinalenga kuwashawishi wananchi wasimchaguwe mpinzani wake.

Dk. Tulia pamoja na wapambe wake wamekuwa wakidai kuwa wagombea wa vyama vya upinzani kikiwamo CHADEMA ambacho kinawakilishwa na Sugu kuwa hawana hoja na badala yake wana 'vihoja'.

Vilevile Dk. Tulia amekuwa akidai Sugu na wabunge wengine wa upinzani walikuwa wanakimbia vikao vya bunge lililopita kwa visingizio mbalimbali ikiwamo bunge la bajeti, hivyo wananchi hawatakiwi kumchagua.

Kwa upande wake, Sugu na wapambe wake wamekuwa wakimponda Dk. Tulia kuwa akiwa Naibu Spika wa Bunge lililopita ndiye aliyeshirikiana na wabunge wa CCM kuzuia Bunge lisionyeshwe mubashara.

Sugu amekuwa akiwaeleza wananchi kuwa endapo Dk. Tulia angeruhusu bunge hilo lionyeshwe wananchi, wangemuona wakati anachangia mambo mbalimbali, hivyo asingekuwa na sababu ya kutembea na mikanda ya video na sauti.

## Samia awaonya wanaCCM wenye 'vidomo'

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amewaonya wanachama wa CCM, Wilaya Kyela wenye vidomodomo vya ufitinishi waache mara moja katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Akizungumza na mamia ya wananchi jana kwenye mkutano wa kampeni, uwanja wa John Mwakangale mjini Kyela, alisema wakati anakuja katika wilaya hiyo alisikia maneno mengi sana, lakini hali aliyoiona ni mtazamo tofauti.

"Niliyoyaona leo (jana) hapa yamenipa moyo sana na niwaombe sana kama alivyosema kaka yetu, Dk. Harrison Mwakyembe, wenye vidomodomo vya ufitinishi hebu sasa wafumbe midomo, tuache wote tushirikiane ili kuivusha Kyela yetu," alisema.

Samia alisema Kyela haina historia mbaya na CCM hivyo wasiende kuitia doa kwenye uchaguzi mkuu na kuwaomba wananchi wa Jimbo la Kyela washikamane na kumpigia kura nyingi rais, mbunge na madiwani wa CCM.

Alisema serikali imeandaa mambo mengi ya kuyafanya katika Wilaya ya Kyela, lakini kama jimbo hilo litachukuliwa na upinzani yote yaliyopangwa hayataletwa kwa sababu yakifanyika mbunge wa upinzani atakayekuwapo atasema yeye kayafanya, lakini ameyafanya kwa nguvu na mgongo wa CCM.

"Mkifanya tofauti maendeleo hayatakuja tena Kyela nawaambia na wala siwadanganyi, hatuwezi kumpa sera zetu mpinzani haiwezekani, kwa hiyo muende mkashikamane mpige kura kwa CCM ili maendeleo yaendelee kuletwa Kyela," alisema.

Vilevile, alisema katika suala la utawala bora, serikali ya CCM itaweka mazingira mazuri ya kuishi na vyama vya upinzani, lakini viiishi kwa heshima na kutambua kuwa CCM ndio Baba lao.

Kwa upande wake Mbunge anayemaliza muda wake Dk. Mwakyembe, alisema tatizo kubwa la siasa katika Wilaya ya Kyela ni wapambe ambao wanatumia muda mwingi kuchonganisha mambo.

"Kyela tatizo ni wapambe, anayegombea hapa ni Mlaghila (Ally Mlaghila), naomba hawa ambao kazi yao ni kuchonga maneno tu watafutiwe mashamba wakalime, " alisema Dk. Mwakyembe huku akishangiliwa na mamia ya wananchi waliohudhuria mkutano huo.

Dk. Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, alisema Kyela ina deni kubwa kwa Rais Dk. John Magufuli kutokana na mambo makubwa ya maendeleo aliyofanya kwa kutekeleza miradi mbalimbali yenye thamani ya mabilioni ya fedha na ilitakiwa apelekewe magunia tu ya kura kama shukrani kwake.

Aliongeza kuwa wakati wa serikali ya awamu ya nne, mawaziri waliokuwa wanahusika na Wizara ya Ujenzi, walikataa kuijenga barabara ya Kikusya-Matema kwa madai kuwa haina tija kwa taifa, lakini baada ya Rais Magufuli kuingia madarakani akaamuru ijengwe na imetumia zaidi ya Sh. bilioni 67.

"Niwaombe wana Kyela, maendeleo hayafanani na mtoto wa mbuzi ambaye akizaliwa leo anaanza kutembea, tuvute subira mazuri zaidi yanakuja," alisema.

TANGAZO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NYASA DISTRICT COUNCIL**

# FINANCIAL STATEMENTS OF NYASA DISTRICT COUNCIL AS AT 30TH JUNE, 2019

**STATEMENT OF CONSOLIDATED FINANCIAL POSITION**
**AS AT 30 JUNE 2019**

| | Notes | 2019 TZS | Restated 2018 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 20 | 1,099,470,974 | 2,333,600,844 |
| Receivables and prepayments | 21 | 762,751,486 | 46,632,108 |
| Inventories | 22 | 114,980,487 | 59,126,700 |
| | | **1,977,202,947** | **2,439,359,652** |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 27 | 20,000,000 | 20,000,000 |
| Property, plant and equipment | 28 | 35,671,917,890 | 32,402,760,823 |
| | | **35,691,917,890** | **32,422,760,823** |
| Non-current assets held for sale | | - | - |
| **TOTAL ASSETS** | | **37,669,120,836** | **34,862,120,475** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 23 | 246,494,203 | 440,944,165 |
| Employee benefits | 24 | 1,025,594,252 | 995,562,596 |
| Deferred income recurrent(Grant) | 11 | 123,258,649 | 503,775,558 |
| | | **1,395,347,104** | **1,940,282,319** |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred income capital (Grant) | 25 | 953,664,797 | 2,019,029,239 |
| | | **953,664,797** | **2,019,029,239** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **2,349,011,901** | **3,959,311,558** |
| **NET ASSETS** | | **35,320,108,936** | **30,902,808,917** |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated Surplus | | 35,300,108,935 | 30,882,808,917 |
| Minimum Compulsory Reserve (LGLB) | | 20,000,000 | 20,000,000 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **35,320,108,935** | **30,902,808,917** |

**Hon. Alto A. Komba - District Chairman** ..............................

**Jimson P. Mhagama District Executive Director** ..............................

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NYASA DISTRICT COUNCIL**
**CASH FLOW STATEMENT**
**FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2019**

| | Note | 2019 TZS | 2018 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Taxes | 33a | 312,668,872 | 424,119,151 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 33b | 155,636,608 | 182,449,691 |
| Exchequers/transfers/subsidies from/(to) other Government entities | 33c | 14,379,526,922 | 3,710,438,898 |
| Revenue from exchange transactions | 33d | 146,923,402 | 67,425,503 |
| Other revenue | 33e | 331,165,429 | 90,649,711 |
| **Payments** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 33f | (12,549,702,012) | (1,139,837,386) |
| Supplies and consumables used | 33g | (1,566,457,281) | (561,164,499) |
| Maintenance expenses | 33h | (174,078,343) | (172,654,931) |
| Grants/subsidies/other transfer payments | 33i | (1,122,233,398) | (2,636,591,238) |
| Interest Epenses | 18 | - | (70,000) |
| Other expenses | 19 | (67,611,409) | (11,774,875) |
| Changes in deposits | 33j | (20,651,837) | 29,524,267 |
| **Cash generated from operations** | | **(174,813,048)** | **(17,485,708)** |
| Interest paid | | - | - |
| **Net cash from operating activities** | | **(174,813,048)** | **(17,485,708)** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Purchase of Property, Plant and Equipments | 31 | (4,331,034,580) | (2,854,974,856) |
| Acquisition of Investmensts | | - | - |
| **Net Cash from Investing activities** | | **(4,331,034,580)** | **(2,854,974,856)** |
| **Cash flows from Financing activities** | | | |
| Proceeds from borrowings | | - | - |
| Reccurent grants reclassified into development grants | | - | - |
| Development Grants Received | 31 | 3,271,717,759 | 2,761,733,987 |
| Grants refunded/transferred | | - | - |
| **Net cash used in financing activities** | | **3,271,717,759** | **2,761,733,987** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | **(1,234,129,869)** | **(110,726,577)** |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | | **2,333,600,843** | **2,444,327,420** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | 20 | **1,099,470,974** | **2,333,600,843** |

**Hon. Alto A. Komba - Dictrict Chairman** ..............................

**Jimson P. Mhagama District Executive Director** ..............................

32

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NYASA DISTRICT COUNCIL**
**STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE**
**FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2019**

| | Notes | 2019 TZS | Restated 2018 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 486,864,596 | 424,119,151 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 305,350,619 | 150,764,741 |
| Amortisation of recurrent grants | 11 | 14,949,410,812 | 15,822,478,360 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 547,118,614 | 67,425,503 |
| Revenue from Non- exchange transactions | 25 | 4,331,034,580 | 2,719,835,277 |
| Other own source revenue | 13 | 484,480,009 | 122,334,661 |
| | | **21,104,259,231** | **19,306,957,693** |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 14 | 12,579,733,668 | 14,147,250,320 |
| Supplies and consumables used | 15 | 1,782,730,642 | 1,522,063,582 |
| Maintenance expenses | 16 | 135,069,572 | 147,313,067 |
| Grants and other transfer payments | 17 | 1,122,233,398 | 1,489,668,246 |
| Interest Epenses | 18 | - | 70,000 |
| Other Expenses | 19 | 67,611,409 | 11,774,875 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 28 | 999,580,522 | 1,707,944,452 |
| Impairment of property plant and equipment | 29 | - | - |
| Amortisation of intangible assets | | - | - |
| | | **16,686,959,212** | **19,026,084,542** |
| Share of associates surplus/(deficit) | | - | - |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | **4,417,300,019** | **280,873,151** |

**Hon. Alto A. Komba - District Chairman** ..............................

**Jimson P. Mhagama District Executive Director** ..............................

**2.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**

To Hon. Chairperson of the Council,
Nyasa District Council,
P.O. Box 135,
MBAMBABAY.

**2.1 Report on the Audit of Financial Statements for the financial year ended 30th June, 2019**

**Unqualified Opinion**

I have audited the accompanying Financial Statements of Nyasa District Council which comprise the statement of Financial Position as at 30th June, 2019 and the Statement of Financial Performance, the statement of changes in net assets/equity the cash flow statement and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the notes to the Financial Statements, including a Summary of Significant Accounting Policies as set out in part 3 of this audit report.

In my opinion, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the financial position of Nyasa District Council as at 30th June, 2019, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSASs) accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act 1982 (revised 2000).

Charles E. Kichere
**CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**
**31st March, 2020**

National Audit Office,
Audit House,
4 Ukaguzi Road,
P.O. Box 950,
41104 TAMBUKARELI,
DODOMA.
Tel: 255 (026) 2321759,
Fax: 255 (026) 2117527,
E-mail: ocag@nao.go.tz
Website: www.nao.go.tz

AUDITOR GENERAL

Controller and Auditor General AR/ LGA/VT/82N5/2018/19

215912302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maonyesho ya wachimbaji, wajasiriamali yawape fursa

WADAU mbalimbali wameratibu, kuendesha na kufadhili maonyesho ya tatu ya uwekezaji wa sekta ya madini, yanayofanyika katika viwanja vya Bombambili mjini Geita.

Ni maonyesho ambayo kwa kiasi kikubwa tunaamini kuwa yana umuhimu mkubwa katika kuwafanya wachimbaji wadogo wa madini na wajasiriamali kuwa na ujuzi na uelewa katika kufanya shughuli za kibiashara na ufanisi.

Tunasema hivyo kwa sababu maonyesho hayo yanakwenda sambamba na kuwapa mafunzo maalumu wajasiriamali na wachimbaji yanayolenga kuwajengea uwezo wa kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kwa viwango shindani vya kimataifa.

Maonyesho hayo ya siku saba zikiwamo siku tatu za mafunzo hayo, itakuwa ni fursa muhimu kwa makundi hayo kunufaika kwa mambo mengi, hususani ujuzi utakaowasaidia kuboresha shughuli zao.

Miongoni mwa vikwazo ambavyo vimekuwa vikitajwa mara kwa mara kuwa kikwazo kwa wachimbaji madini wadogo na wajasiriamali ni kukosa mitaji, elimu na ujuzi, hivyo kujikuta wakikwama kufikia malengo na ndoto zao.

Kwa hiyo tunaamini kuwa waliopata fursa hiyo adhimu wataitumia kujifunza mambo mbalimbali pamoja na kusikiliza na kuzingatia ushauri watakaopewa na wataalamu na watu wengine watakaokwenda kutembelea maonyesho hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Gabriel, akizungumza wakati wa ufunguzi wa utoaji wa mafunzo hayo, alitoa wito kwa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo kuzingatia kanuni za utunzaji wa fedha na heshima ya matumizi ili kulinda na kukuza mitaji yao.

Utunzaji fedha na matumizi yake, imekuwa ikielezwa kuwa ni kikwazo kwa wachimbaji wadogo wa wajasiriamali kupata maendeleo na kukua kibiashara.

Inaelezwa kuwa wachimbaji wadogo wengi pamoja na wafanyabiashara wadogo wanapopata fedha hawana utaratibu mzuri wa kuzipangia matumizi, badala yake kuzitumia kwenye starehe kisha baadaye kujikuta wakiwa wanakwama kuendelea.

Ni wakati sasa kwao kuelewa kuwa fedha hizo wanapaswa kuzitunza kwenye taasisi rasmi za fedha sambamba na kuzitumia taasisi hizo kwa ajili ya kupata mikopo isiyo na riba kubwa, ambazo zinasababisha wakopaji mkufilisiwa mali zao wanaposhindwa kufanya marejesho.

Jambo la kutia matumaini ni kuwa miongoni mwa wadai wanaofadhili na waratibu wa maonyesho haya ni taasisi za fedha, hivyo ni matarajio yetu kuwa washiriki watapata elimu ya kutosha kuhusiana na kanuni bora za utunzani na heshima ya matumizi ya fedha.

Fursa ambayo makundi hayo yametangaziwa ni ya kupelekwa nje ya nchi kupata uzoefu iliyotolewa na taasisi moja ya fedha nchini, huku serikali ikisema imeunga mkono mpango huo wa kuwasafirisha wachimbaji wadogo na wajasiriamali wa sekta ya madini kwenda katika mataifa yanayofanya vizuri kwenye sekta ya madini ikiwamo Zimbabwe, Ghana na Msumbiji.

Lengo la mpango huo limeelezwa ni kuwawezesha wajifunze na kutafuta namna bora zaidi ya kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kiwango cha kimataifa.

Akizungumza alipotembelea banda la taasisi hiyo, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema pamoja na kushirikiana kufanikisha ziara hizo, serikali itashauriana na wadau wote wakiwamo wachimbaji hao ili kuongeza tija katika safari hizo.

Alisema serikali ipo tayari kushirikiana na pande zote wakiwamo wachimbaji ili kufahamu nchi sahihi ambazo zimefanya vizuri kwenye sekta hiyo ili walengwa wapate wasaa wa kujifunza mambo ambayo yatawasaidia zaidi.

Tunashauri kwamba wachimbaji wadogo wa madini na wajasiriamali waendelee kuwezeshwa kwa mafunzo mara kwa mara kupitia maonyesho na njia zingine ambazo zitaonekana zinafaa kuwakutanisha, lengo likiwa ni kuwapa uelewa na uzoefu wa kufanya biashara kwa tija na ufanisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kumbukeni maisha baada ya uchaguzi

Na Sabato Kasika

MAJUKWAANI joto la kampeni za uchaguzi mkuu linazidi kupanda kwa wagombea wa urais, ubunge na udiwani wa vyama mbalimbali kujinadi kwa wapigakura.

Uchaguzi mkuu unatarajiwa kufanyika Oktoba 28, ukiwa ni wa sita tangu kurejeshwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na kufanya uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo mwaka 1995.

Tume Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilipuliza kipenga cha kuanza kampeni takribani mwezi mzima sasa, zikianza rasmi hizo Agosti 26, na kuhitimishwa Oktoba 27 na kufuatiwa na uchaguzi mkuu Jumatano Oktoba 28, 2020.

Lakini, wakati kampeni zinaendelea, ni muhimu kuwakumbusha wanasiasa kuzingatia mambo ambayo yanaelekezwa na NEC, kwa lengo la kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na utulivu.

Yako mambo kadhaa ambayo NEC inawataka wanasiasa kuyaepuka ili mchakato wote kuanzia mwanzo hadi mwisho uhitimishwe kwa amani na utulivu.

Wagombea wakiendelea kujiweka kando na kutumia lugha zinazoweza kutibua amani, utulivu na mustakabali wa uchaguzi.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Willson Mahera, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, anawahimiza wanasiasa kuzingatia maadili ya uchaguzi, ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa.

NEC inaweka wazi kuwa, haitaki kampeni zenye matusi ama za kuhatarisha amani ya nchi na hilo pia linatiliwa mkazo na serikali, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Jeshi la Polisi.

Inataja baadhi ya mambo ambayo yanayokiuka maadili ya uchaguzi ikiwamo lugha za kashfa na matusi kwa wagombea na viongozi wa vyama wakati wa kampeni.

Mengine ni kuzidisha muda wa kampeni, ukiukwaji wa ratiba ya kampeni, maandamano ya wafuasi wa vyama vya siasa yasiyokuwa na vibali kabla na baada ya muda wa kampeni.

Aidha, wafuasi wa vyama vya siasa pia hatakiwi kuharibu mabango ya wagombea wa vyama vingine watendaji wa serikali kutoingilia shughuli za vyama vya siasa, kutofanya vurugu dhidi ya vyama vingine na wagombea.

Hairuhusiwi kubandika picha za wagombea juu ya picha za wagombea wa vyama vingine, wafuasi wa vyama na wagombea kutoingilia mikutano ya wagombea wa vyama vingine na kutoa kauli zisizoweza kuthibitishwa.

Lengo la NEC kuhimiza hayo yote ni kutaka kuhimiza amani ili kuhakikisha kampeni zinafanyika na kuhitimishwa vizuri na hatimaye Oktoba 28 Watanzania wachague viongozi wanaowataka.

Kutokana na maelekezo hayo, NEC inatarajia kwamba vyama vyote ambavyo vimeweka wagombea vitazingatia hayo na kuhimiza wanachama wake kufanya hivyo, kwa kuwa Watanzania wanataka ilani na sera.

Hivyo ni wajibu wa kila mwanasiasa kutambua kuwa, kuna maisha baada ya uchaguzi, hivyo ajenda muhimu kwao, waepuke siasa za majitaka ambazo zinaweza kuwaigiza kwenye matatizo yasiyo ya lazima.

Uzoefu unaonyesha kuwa kila ifikapo wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, kuna baadhi ya wanasiasa, ambao 'huwashambulia' wenzao kwa maneno makali na wengine kutoleana matusi.

Katokana na mwendelezo huo wa siasa za majitaka, wakati mwingine mashabiki na wafuasi wa vyama vya siasa 'hushambuliana' na kuumizana, wakisahau kwamba, kuna maisha baada ya uchaguzi.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema wanasiasa kuanzia wagombea, wanachama na mashabiki wa vyama vya siasa kuzingatia kile ambacho kinaelekezwa na NEC ili kuweka mbele maslahi ya taifa.

Wagombea wa urais, ubunge na udiwani, wameaminiwa na vyama vyao na kupewa dhamana ya kuwania nafasi hizo, hivyo matarajio ya Watanzania ni wao kuzingatia kanuni, sheria, maadili na taratibu zote za uchaguzi.

Kipindi cha kampeni za uchaguzi ni muhimu kunadi ilani na sera na kukwepa matumizi mabaya ya lugha ikiwamo matusi na kejeli, kwa kuwa kwa kufanya hivyo wataepusha aina yoyote ya uvunjifu wa amani.

Kila chama kimeingia katika kampeni kikiwa na ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020 hadi 2025, yaliyomo humo ndiyo yapewe kipaumbele, ili Watanzania wajue ni nini mgombea amejipanga kuwafanyia.

Hiyo ndiyo kiu ya Watanzania, siyo kampeni za matusi ama mambo mengine yanayofanana nayo. Hivyo ni wajibu wa wadau wote wa uchaguzi kuhimiza kampeni za kistaarabu ili hatimaye wapigakura wafanye uamuzi sahihi.

Kikubwa zaidi ni kutambua kwamba, kuna maisha baada ya uchaguzi, hivyo wanasiasa wanapogombania fito kwa ajili ya kuijenga Tanzania, wasiwe nje ya kile ambacho kinaelekezwa na NEC.

MAKALA MAALUM



Rais John Magufuli akizindua Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma Aprili 5, 2019. Wa pili kushoto ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako.

# VETA nayo yajiunga uchumi viwanda kwa mtaji wataalamu

## ■ *Wilaya mafichoni zasogea kileleni*
## ■ *Vyuo vipya 25, ajira kwa sekta 13*

**Na Enock Charles**

HATIMAYE azma ya nchi kuingia uchumi wa kati imefikiwa mwaka huu, ikiwa imebaki miaka mitano ya utekelezaji wake.

Juni 1999, Tanzania iliandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo pamoja na mambo mengine, ililenga kupunguza nusu ya wananchi wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Katika kuhakikisha azma hiyo ya kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda, mafunzo ya ufundi stadi yameendelea kuhitajika kwa wingi katika maeneo mbalimbali nchini, huku kukiwa na mwamko mkubwa wa wananchi hususan vijana kutambua kuwa ufundi stadi ni mkombozi kwao kuajiriwa, kuajiri na kuajiri wengine.

Waendeshaji wakubwa wa viwanda ni wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi. Vilevile, watu wenye ujuzi wa ufundi stadi ndiyo wanaochangia juhudi za serikali kwa kufungua viwanda vidogo vidogo.

Kwa kutambua umuhimu wa mafunzo hayo, serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha mafunzo ya ufundi stadi yanawafikia na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi.

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Dk. Pancras Bujulu, anasema lengo la serikali ni kuwa na chuo cha ufundi stadi katika kila mkoa na kila wilaya nchini ifikapo mwaka 2025, ili kuhakikisha inazalisha rasilimali watu ya kutosha yenye ujuzi, kwa ajili ya maendeleo endelevu ya viwanda.

"Mwitikio wa wananchi kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi umekuwa mkubwa sana ndiyo maana tumekuwa tukipokea maombi mengi ya vijana kutaka kujiunga na mafunzo haya. Tunataka kuhakikisha kuwa watu wote wenye uhitaji wa mafunzo, wanayapata kwa urahisi, ili wajipatie ujuzi wa kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi," anasema.

Dk. Bujulu anasema katika ngazi ya wilaya, serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo vipya vya VETA vya Namtumbo, Urambo, Ndolage, Muleba, Nyamidaho, Nkasi, Ileje, Kanadi, Itilima, Samunge, Ngorongoro, Gorowa, Babati na Mabalanga, Kilindi.

Anabainisha kuwa Chuo cha VETA Chato na Kitangali (Newala) viko kwenye hatua za mwisho kukamilishwa huku ujenzi katika Wilaya za Kasulu, Nyasa, Ruangwa na Kongwa ukiendelea vizuri.

Mkurugenzi huyo anaongeza kuwa vyuo vingine 25 vya VETA vinaendelea kujengwa katika Wilaya za Chunya, Kilindi, Korogwe, Ukerewe, Igunga,

**Dk. Bujulu anasema katika ngazi ya wilaya, serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo vipya vya VETA vya Namtumbo, Urambo, Ndolage, Muleba, Nyamidaho, Nkasi, Ileje, Kanadi, Itilima, Samunge, Ngorongoro, Gorowa, Babati na Mabalanga, Kilindi.**

Pangani, Kishapu, Rufiji, Uyui, Kwimba, Bahi, Mafia, Longido, Mkinga, Uvinza, Ikungi, Iringa Vijijini, Lushoto, Mbarali, Monduli, Buhigwe, Ulanga, Masasi, Butiama na Chemba, ambavyo vinajengwa kwa kutumia rasilimali na nguvukazi ya VETA kwa utaratibu wa 'Force Account'.

Pamoja na ujenzi wa vyuo vya wilaya, mkurugenzi huyo anasema serikali inajenga vyuo vya VETA vya Mikoa ya Rukwa, Geita na Njombe. Chuo kingine kinachojengwa ni cha Mkoa wa Kagera kupitia ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Dk. Bujulu anasema ujenzi huo wa vyuo unaenda sambamba na uboreshaji wa karakana pamoja na ununuzi na usimikaji wa vifaa vya mafunzo kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanatolewa kwa ubora hasa kwa kuzingatia kuwa utoaji mafunzo ya ufundi stadi unajikita zaidi kwenye vitendo.

Anatoa mfano wa kiwanda cha kisasa cha kutengeneza samani cha VETA, kilichoko katika Chuo cha VETA Dodoma, kilichozinduliwa Septemba 2019, kwamba kina vifaa vyote muhimu na kisasa.

Karakana nyingine zilizoboreshwa ni pamoja na Karakana za Umeme wa Viwandani za VETA Tanga na Mwanza; Karakana ya Ushonaji VETA Pwani; Karakana za Ufundi wa Zana za Kilimo za VETA Kihonda na Arusha; Karakana ya Uchoraji wa Ramani za Majengo ya VETA Moshi na Karakana za Umeme, na Uchomeleaji na Uungaji Vyuma za VETA Mtwara.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa, pamoja na mkakati wa ujenzi wa vyuo vipya, VETA imekuwa ikibuni mafunzo mbalimbali yanayoendana na mahitaji kwenye jamii, akitolea mfano mafunzo ya umahiri wa ufundi wa simu za mkononi yanayotolewa na VETA kupitia chuo chake cha TEHAMA VETA Kipawa kwa lengo la kuwawezesha mafundi simu kufanya kazi zao kwa weledi na uadilifu.

Dk. Bujulu anabainisha kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2021, matarajio ni kuwa na jumla ya vyuo 72 vinavyomilikiwa na VETA kutoka 37 vya sasa na hivyo kuongeza udahili kutoka 704,000, kwa sasa hadi kufikia wanafunzi milioni moja kwa mwaka.

Anasema, vyuo vyao vya ufundi stadi vinatoa mafunzo katika fani zaidi ya 80 zilizogawanywa katika sekta za ajira 13, ambazo ni ufundi mekanika; ufundi umeme; ufundi ujenzi; ufundi magari na mitambo; huduma za biashara; mavazi na nguo; usafirishaji na uchukuzi; uzinduzi (utafutaji, uchimbaji na uchakataji madini); uchapaji; urembo na ususi; kilimo na usindikaji chakula; ukarimu na utalii pamoja na fani za sanaa.

# Biteko aitaka BRELA kuwashughulikia vishoka

**Na Mwandishi Wetu, GEITA**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ameutaka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutatua changamoto ya vishoka wa mitandaoni, ambao wamekuwa wakiwasumbua wafanyabiashara wanaotaka kusajili majina na alama za biashara.

Biteko alitoa agizo hilo jana alipotembelea banda la BRELA katika maonyesho ya tatu ya uwekezaji wa sekta ya madini, yanayofanyika katika viwanja vya Bombambili mjini hapa.

"Naipongeza BRELA kwa kutatua tatizo la kampuni hewa na migogoro ya kampuni. Changamoto kubwa ambayo bado ni vishoka, ambao wanasumbua katika mitandao. Naomba mwendelee kulishughulikia hilo," alisema Biteko.

Pia, aliipongeza BRELA kwa kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Madini anayoiongoza na kuongeza kuwa taasisi hiyo imekuwa ikitoa ushirikiano wa haraka mara inapohitajika kufanya hivyo.

Alitolea mfano wa ushirikiano uliofanywa na BRELA kwa Wizara ya Madini, ambao umefanikisha kutatua tatizo la kampuni hewa na migogoro ya kampuni hususani kampuni ya uchimbaji madini ya Nyarugusu. Katika mgogoro huo, alisema BRELA imetoa ushirikiano wa kutosha katika kuutatua.

Pia, aliipongeza BRELA kwa kazi nzuri ya kuhakikisha matatizo na changamoto zinatatuliwa, kwa wakati hasa baada ya kuweka mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao. Alisema mfumo huo umepunguza baadhi ya changamoto kwa wafanyabiashara na kupata huduma haraka na kwa wakati

Waziri Biteko alisema matarajio ya serikali ni kuona wafanyabiashara wa madini, hususani wachimbaji wadogo, wanaachana na uchimbaji wa kutumia majina yao na badala yake wanatakiwa kusajili kampuni, ambazo zitawaongezea tija na kulipa kodi na kuchangia katika pato la taifa.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Sarah Chiwamba (katikati), akikagua bidhaa za wajasiriamali katika maonyesho yaliyofanyika mjini Liwale, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mabadiliko ya sheria yapaisha sekta ya madini

**Na Mwandishi Wetu, GEITA**

SEKTA ya madini imefanikiwa katika usimamizi wake kutokana na mabadiliko ya sheria yaliyofanywa mwaka 2017, hivyo kuifanya kuongoza katika ukuaji kwa asilimia 17.7.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Alisema, sekta ya madini imeongoza kwa ukuaji kwa asilimia 17.7 na ndiyo inayoongoza kwa kuiletea serikali fedha za kigeni.

Biteko alisema sekta ya madini inaongoza kwa kusafirisha bidhaa kwenda nje ya nchi na kwamba asilimia 51.9 ya bidhaa zote zinazosafirishwa nje ya nchi zinatokana na sekta hiyo.

Pia alisema, mapato yatokanayo na madini yamepanda kutoka Sh. bilioni 168 kwa mwaka mpaka Sh. bilioni 528.

Alisema katika mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017, kuna kipengele kinachoeleza kuwa kampuni zote zinazochimba madini nchini lazima zifungue akaunti zake ndani ya nchi.

Kampuni ya Barrick iliyoingia ubia na serikali na kutengeneza kampuni ya pamoja ya Twiga, imefungua akaunti zake zote nchini na mkataba huo ulitiwa saini Januari 24, mwaka huu.

Pia, Waziri Biteko alisema makinikia yanayosafirishwa nje ya nchi yanakuwa yameshanunuliwa nchini na kuyapima kwenye maabara tatu tofauti, ili kujiridhisha kiwango na aina za madini yaliyomo kwenye makinikia hayo na fedha zote zinawekwa kwenye banki za hapa nchini tofauti na ilivyokuwa awali.

# Shule 151 Rorya zamwagiwa pesa

**Na Mwandishi Wetu, SHIRATI**

SHULE 151 wilayani Rorya mkoani Mara, zikiwamo 120 za msingi na 31 za sekondari zimenufaika na mpango wa elimu, bila malipo uliotekelezwa tangu 2015.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wakazi wa mji wa Shirati, kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa mpira wa Obwere.

Alisema, Sh. bilioni 3.3 zilitolewa kwa ajili ya shule za msingi 120 kwa ajili ya kufanya ukarabati, masuala ya utawala, michezo, mitihani na posho kwa maofisa elimu kata na walimu wakuu.

"Kwa upande wa shule za sekondari, Sh. bilioni 2.5 zilitolewa kwa shule 31 kwa ajili ya fidia ya ada, chakula kwa shule za bweni na posho ya madaraka kwa wakuu wa shule," alisema.

Kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya shule ulivyofanywa kupitia Mpango wa Lipa Kutokana na Matokeo (EP4R), Majaliwa alisema, Sh. bilioni 1.2 zilitolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya madarasa, mashimo ya vyoo na nyumba za walimu kwa shule za msingi.

Alizitaja baadhi ya shule za msingi zilizonufaika na mpango huo kuwa ni Mori, Nyanduga, Buchuri, Kondo, Saye, Masonga, Kyaro, Kitembe, Bubombi, Oliyo B, Dagopa, Nyabi, Ratia, Kotwo, Muchirobi, Manyara, Ochuna na Nuamaguku.

"Kwa upande wa shule za sekondari, zimetumika Sh. milioni 777.8, kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwamo maabara, madarasa, mabweni na vyoo kwa shule za Bukama, Mirare, Ngasaro, Nyamunga, Buturi, Goribe, Nyathorogo, Nyamtinga na Waningo," alisema.

Majaliwa ambaye yuko mkoani Mara kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Rais John Magufuli, alitumia fursa hiyo kuwaombea kura mgombea ubunge wa Jimbo la Rorya, Jafari Chege, mgombea udiwani wa Kata ya Mkoma, Ayoi Sonde na wale wa udiwani katika jimbo hilo.

Akizungumzia utekelezaji wa Ilani ya CCM kwenye sekta ya nishati, Majaliwa alisema vijiji 74 kati ya vijiji 87 vya Wilaya ya Rorya vimepata umeme.

Alivitaja vijiji vilivyobaki visivyo na umeme kuwa ni Thabache, Nyabikondo, Nyahera, Bugendi, Burere, Wamaya, Nyabiwe, Masike, Busanga, Nyihara, Kyanyamsana, Nyamusi na Oliyo.

## TBS yatengeneza viwango vya ubora sekta ya madini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetengeneza zaidi ya viwango 100 ambavyo vitatumika kudhibiti ubora katika sekta ya madini kwenye masuala ya utafiti, uchimbaji na uchenjuaji.

Akizungumza katika maonyesho ya tatu ya madini na teknolojia yanayoendelea katika viwanja vya Magogo mkoani Geita jana, msemaji wa TBS, Roida Andusamile alisema:

"TBS imeandaa viwango ambavyo vinahakikisha usalama katika sekta ya madini unaimarika na kuifanya sekta hii kuendelea kuwa mchangiaji mkubwa katika pato la taifa."

Andusamile aliongeza: "Viwango hivi vimeandaliwa kudhibiti viwango kwa wachimbaji wakubwa na wadogo. Sababu ya kuleta viwango hivi ni kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji madini zinaendeshwa katika mazingira salama na yenye ubora."

"Kwa upande wa kipekee, shirika letu la viwango lina jukumu la kuchukua hatua za kudhibiti ubora wa bidhaa, huduma na mazingira kwa nchi nzima. Ndio maana tulianzisha viwango hivi kudhibiti ubora katika sekta ya madini," aliongeza Andusamile.

Kwa upande wake, Ofisa Viwango wa TBS katika Madini, Filbeta Magidanga, alisema: "Tunajivunia kuandaa viwango zaidi ya 100 ambavyo vitadhibiti na kuimarisha ubora kwenye sekta ya madini."

Aliongezea: "Viwango hivi vinatengenezwa na Kamati ya Viwango TBS ambayo ina jukumu la kuandaa na kutengeneza viwango katika utafiti wa madini, uchimbaji, upimaji na uchenjuaji."

## Waaswa kupeleka watoto shule za ufaulu

**Na Yasmine Protace**

WAZAZI na walezi, wametakiwa kutokimbilia shule zenye ufaulu kwa ajili ya kuwapeleka watoto wao kusoma, bali kinachotakiwa ni kuwatafutia shule ambazo zinawajenga watoto kimaadili.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shule ya St. Mark's, Peter Mutembei, katika mahafari ya 17 ya kidato cha nne ya shule hiyo.

Alisema baadhi ya wazazi wanakimbilia shule zenye ufaulu, lakini wanashindwa kuelewa kuwa kuna shule zina ufaulu, lakini haziwajengei watoto maadili.

"Kabla ya kumpeleka mtoto shule mzazi inatakiwa ufuatilie shule hiyo ina maadili au haina na kama haina usikimbilie sifa za ufaulu pekee na ukampeleka mtoto," alisema.

Aliongeza kuwa kama mtoto atakuwa hana maadili na akafaulu vizuri mitihani yake, lakini anapopata ajira hawezi kufanya kazi vizuri kutokana na kutokuwa na maadili mema.

Alisema kuwa shule yao kutokana na kuwafundisha maadili mema, wanafunzi wao mpaka sasa hakuna mtoto wa kike aliyeacha shule kwa kupata ujauzito. Alisema shule yao imeanzisha sera ya usalama kwa watoto wakiwa ndani ya shule na nje ya shule.

"Tumeanzisha sera yetu, tunawalinda watoto na matendo ya usalama nje ya shule na ndani ya shule," alisema.

# Vita dhidi ya magonjwa ya mifugo kuendelea

**Na Elizabeth Zaya**

**Tayari Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kilichopo mkoani Tanga kimeshapata njia nzuri na rahisi ya kutokomeza magonjwa ya mifugo.**

SERIKALI imesema itaendelea kukabiliana na magonjwa ya mifugo nchini kwa kutumia njia ya chanjo pamoja na kutokomeza wadudu wakiwamo mbung'o ambao wanaathiri afya ya wanyama.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema taasisi za serikali zinazosimamia sekta hiyo zimekuwa zikifanya kazi kubwa ya kufanya utafiti na kutafuta tiba ya magonjwa ya mifugo nchini.

Prof. Gabriel alisema tayari Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kilichopo mkoani Tanga kimeshapata njia nzuri na rahisi ya kutokomeza magonjwa ya mifugo.

Alisema Lengo ni kuhakikisha wafugaji wanapata tija ya ufugaji na wanaondokana na kufuga kwa mazoea na kuingia katika ufugaji wa kisayansi bila kuwa na magonjwa yanayoathiri ustawi wa mifugo yao.

Ofisa Utafiti wa Mifugo kutoka TVLA mkoani Tanga, Peter Lucas, alisema miongoni mwa njia rahisi ambazo wafugaji wanatakiwa kuzitumia katika kutokomeza mbung'o ni pamoja na kuweka mtego wa kuwakamata pamoja na njia ya kuweka dawa maalum ya kuwaua kwa kutumia vitambaa vyenye rangi ya bluu na nyeusi kwa sababu huwavutia wadudu.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Mkoa wa Tanga, Dk. Zabron Nziku, alisema kuwa wameanzisha maabara ya kisasa kwa ajili ya kutengeneza virutubisho vya mifugo vinavyotokana na zao la muhogo ambavyo havina gharama kubwa kwa wafugaji.




Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa tatu kulia), akikata utepe kuzindua huduma ya mkopo wa vifaa vya kilimo inayojulikana kama Chukua Trekta Tukalime, inayotolewa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na kampuni zinazouza matrekta nchini za ETC Agro, LonAgro na Agricom, jijini Dar es Salaam jana. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Tanzania yazinoa nchi kinara uzalishaji korosho

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

LICHA ya Tanzania kuzifundisha kilimo cha korosho nchi za Ivory Coast na Nigeria, nchi hizo zinaongoza kwa kuzalisha zao hilo Afrika na duniani na kuizidi Tanzania.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Naliendele kitengo cha Agronomia ya Korosho, Kasiga Ngila, aliyasema hayo jana, kwenye mafunzo ya wakulima wa korosho kutoka Halmashauri za Kilosa na Gairo mkoani Morogoro ambayo yamefanyika wilayani Gairo.

Alisema takwimu ambazo zimepatikana kutoka mtandao wa Kilimo forum.com zinaonyesha Tanzania ni chi ya nne kwa nchi ya Afrika kwa kuzalisha korosho ikitanguliwa na Nigeria inayoongoza kwa kuzalisha tani za ujazo 900,000 kwa mwaka ikifuatiwa na Ivory Coast inayozalisha tani za ujazo 600,000.

Alisema nchi ya tatu kwa kuzalisha korosho barani Afrika ni Guinea Bissau inayozalisha tani za ujazo 400,000 kwa mwaka, ambapo Tanzania inazalisha tani za ujazo 300,000 kwa mwaka.

"Tunajisikia vibaya kuzifundisha nchi hizi kilimo cha korosho kisha wanakwenda kulima na kuzalisha kwa wingi kuliko sisi, ndio maana sasa tumeamua kusambaza elimu kwa wakulima wetu ili na sisi tuongeze uzalishaji," alisema Kasiga.

Kasiga alisema kwa duniani nchi inayoongoza ni Vietnam ikizalisha tani za ujazo milioni 1.2 na ya pili ni Nigeria ikizalisha tani 900,000,India ikizalisha (900,000) na Ivory Coast tani (600,000).

Kwa upande wake akitoa elimu ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima wa Wilaya ya Kilosa na Gairo, Mtafiti wa Magonjwa na Visumbufu vya zao la korosho, Dk. Wilson Nene, alisema sababu inayopelekea kuwapo kwa uzalishaji mdogo wa zao hilo nchini ni pamoja na wakulima kushindwa kutumia mbegu bora za kisasa na badala yake wamekuwa wakitumia mbegu za kienyeji.

# Lori lingine la mafuta lateketea

**Na Mwandishi wetu**

GARI la mafuta lililokuwa linaelekea Burundi, kutokea jijini Dar es Salaam limeteketea kwa moto.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Goodluck Zolote, gari hilo ni lenye namba za usajili T 862 BZS na lenye namba T814 DBZ, na kwamba ajali ilitokea Septemba 20, mwaka huu.

**Gari hilo ni mali ya Interpetrol likiendeshwa na dereva Hamidu Issa, na ajali hiyo ilitokea eneo la Kilosa, mkoani humo.**

Alisema, gari hilo ni mali ya kampuni ya Interpetrol likiendeshwa na dereva Hamidu Issa, na ajali hiyo ilitokea eneo la Kilosa, mkoani humo.

Aidha, alisema kuwa zilifanyika jitihada za kuokoa kiasi kikubwa cha mafuta na kudhibiti moto na kwamba haukuleta madhara yoyote.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, chanzo cha ajali hiyo hakijajulikana, huku akieleza kuwa kumekua na matukio ya mara kwa mara ya magari ya mafuta kuwaka moto na kusababisha madhara makubwa.

"Kumekuwa na wimbi kubwa la matukio ya aina hii kutokea mara kwa mara katika maeneo mbalimbali hapa nchini na mengine yamesababisha maafa makubwa na hata kusababisha vifo vya watu wengi sana, hii ni kutokana na watu kuyakimbilia magari, ili kuchota mafuta pindi tu yanapoanguka," alifafanua.




Waziri wa Madini, Doto Biteko, akipokea cheti cha usajili wa jina la biashara kutoka kwa ofisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mariam Mollel, baada ya kujisajili na kukipata hapohapo kwenye maonyesho ya madini yanayoendelea kwenye viwanja vya Bombambili mkoani Geita juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbwa, paka 300 wapatiwa chanjo

**Na Elisante John,** SINGIDA

ZAIDI ya mbwa na paka 300, wamepatiwa chanjo katika Wilaya ya Iramba mkoani Singida, kupitia Shirika lisilo la Kiserikali la Education for Africa Animal Welfare Organization (EAAW), lenye makao yake jijini Dar es Salaam, ili kukabiliana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Chanjo ya mbwa na paka katika wilaya hiyo ni mwendelezo wa Shirika la EAAW, linalojihusisha na ustawi wa wanyama kwa kuielimisha jamii juu ya haki za wanyama, matunzo na matibabu yake, kuendesha zoezi kama hilo mwaka jana (2019).

Kwa mujibu wa ofisa mifugo na uvuvi Wilaya ya Iramba, Dk. Dotto Thomas, kichaa cha mbwa ni tatizo linaloikabili dunia, kutokana na athari zake kwa binadamu, ambaye maisha huwa hatarini baada ya kung'atwa na mbwa au paka mwenye kirusi cha maradhi ya ugonjwa huo.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Dotto alibainisha kuwa tiba yake ni ghari na nchini hutolewa katika baadhi ya hospitali, huku zahanati na vituo vingi vya afya hususani kwenye maeneo ya vijijini, vikikosa huduma hiyo na hivyo kusabisha wahanga wengi kupoteza maisha.

Dk. Dotto alifafanua kuwa, katika kukabiliana na tatizo hilo, Wilaya ya Iramba na EAAW, walitekeleza zoezi la chanjo kwa siku mbili na kufanikisha mbwa na paka 300 eneo la Kiomboi Mjini, huku mkakati ukiandaliwa kwa ajili ya wilaya yote.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa EAAW, Ayubu Nnko, alitoa rai kwa jamii ya wilaya hiyo kuhakikisha inawapatia mbwa na paka huduma zote muhimu, ikiwamo chanjo kila mwaka, ili kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

# Waajiri wakumbushwa kuwekeza kwa wafanyakazi

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Conrad Msoma, amewakumbusha waajiri kuwekeza kwa wafanyakazi wao kwa kuhakikisha wanakuwa na furaha na amani wanapotekeleza majukumu yao, katika maeneo yao ya kazi.

Msoma alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema, kuna umuhimu wa kuwajali na kuwahakikishia usalama wafanyakazi wanapokuwa kazini kwa kuweka mazingira na mifumo bora ya kazi inayotoa haki kwa kila mfanyakazi.

Akitoa mfano katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa corona, Msoma alisema kilikuwa ni kipimo kwa waajiri katika kuwalinda wafanyakazi wake hususani kwa kubuni mbinu mbadala za kutekeleza majukumu yao bila kujali gharama.

"Kuzingatia maadili, ujumuishi, haki sawa kwa wafanyakazi wote nalo ni jambo la msingi, na haya ndiyo baadhi ya mambo yanayoifanya Kampuni ya SBL kuwa mbele ya waajiri wengine katika soko la ajira hapa nchini," alisema Msoma.

Aliwashauri waajiri kuwa na sera nzuri, ambazo zitakuwa ni rafiki kwa wafanyakazi wote, ambazo pia zitakuwa zinatambua mchango wa wafanyakazi bora.

"Na sisi tunapendelea kutoa kipaumbele kwa mazingira bora ya kazi kwa kuwa huchangia kwa kiwango kikubwa mfanyakazi kuwa na furaha. Kuwa mwajiriwa bora hakumaanishi tu kuwa na sera bora za kazi, bali pia utamaduni mzuri unaomfanya mfanyakazi ajisikie huru na kuona kuwa kampuni inamjali pamoja na kumthamini," alisema Msoma.

"Na kutokana na sera pamoja na taratibu bora za kuwajali wafanyakazi wetu, tumefanikiwa kupata tuzo mbalimbali ikiwamo tuzo za kimataifa, ambazo zimetokana na utendaji uliotukuka katika ngazi ya kitaifa na kimataifa."

## CRDB yakopesha wakulima korosho bil. 1.3/-

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

ZAIDI ya Sh. bilioni 1.335 zilikopeshwa na Benki ya Biashara ya CRDB kwa wakulima 648 wa korosho, katika kipindi cha maandalizi msimu 2020 /2021, ili kuwawezesha kuzalisha mazao ya kutosha na kujiongezea kipato.

Sambamba na mikopo hiyo, pia benki hiyo imeanzisha akaunti maalumu ya Fahaari Kilimo, ambayo haina makato, ili kumwondolea mkulima adha ya akaunti yake kulala anapokuwa hajaingiza fedha katika kipindi cha miezi 24.

Hayo yalisemwa na Meneja Biashara wa Benki hiyo Kanda ya Kusini, Benadeta Mshanga, kwenye mafunzo ya fursa mbalimbali zinazotolewa na CRDB kwa viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika wa wakulima Amcos, na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Tunduru (TAMCU).

Mshanga alisema fedha hizo zilitolewa kwa wakulima, ili kuwasasidia kununulia pembejeo na kufanya maandalizi mengine ya mashamba yao zikiwa ni jitihada za benki hiyo kuunga mkono juhudi za serikali kumkomboa mkulima.

Meneja wa Bodi ya Korosho Tanzania Tawi la Tunduru, Sauri Ally Mokiwa na Ofisa Ushirika wilaya ya Tunduru, Goerge Bisani, walipongeza utolewaji wa mikopo hiyo na kuwataka wakulima na viongozi wa vyama vya msingi kuzitumia fursa hizo kwa uaminifu, ili waweze kunufaika nazo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa niaba ya viongozi hao, Athumani Mjase wa Mkanai Amcos na Mayanga mohammed wa Mrimi Amcos, waliiomba benki hiyo kuangalia uwezekano wa kupunguza riba kwenye mikopo, kupunguza urasimu ambao umekuwa ukichelewesha mikopo.

Mwenyekiti wa TAMCU, Hashimu Mbalaabala, aliwaagiza wenyeviti na makatibu wa VAMCOS kuweka makarani waaminifu, ili waweze kukusanya mazao ya wakulima kwa uaminifu.

# KINAMAMA MPOO...

Ukurasa 12





Ukurasa 14

**THOMAS ISIDORE NOËL SANKARA**

siasa

JUMATANO SEPTEMBA 23, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Tanzania ilipojibu tuhuma za UN haki za binadamu

■ Lawama za 2015 zimepotea, zaibuliwa nyingine



**Na Ani Jozeni**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Profesa Palamagamba Kabudi (pichani), hivi karibuni analazimika kutumia taaluma na diplomasia kujibu hoja za Shirika la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, ambalo limetoa taarifa yake inayoibua lawama kwa Tanzania.

Taarifa hiyo inaelekeza lawama kwa taifa likitaja baadhi ya mambo kuwa ni pamoja na kukiuka haki za binadamu, uhuru wa habari, haki za wapinzani kufanyakazi zao, kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa hivi karibuni.

Hata hivyo, serikali haikutaja tarehe halisi ya taarifa ya UN, ila ilionekana ni ya mwaka huu kwani ingekuwa ya 2019 ingekamilika na kutolewa kabla, labda kwa maelezo ya kukwamishwa na vizuizi vya kuzuka kwa janga la COVID-19. Kimsingi ni taarifa ya mwaka huu na imetolewa wakati Tanzania inajiandaa kufanyika uchaguzi mkuu na wageni wa kimataifa wameruhusiwa kuuangalia.

Majibu ya Waziri Kabudi yalikuwa pia kama yanalenga kutoa maelezo ya ndani na kwa maana hiyo kuwapa tafsiri ya mpangilio wa kufanyika uchaguzi mkuu.

Moja ya maeneo muhimu ya kufanyika uchaguzi na hasa katika uchaguzi mkuu ni kuwapo wagombea tofauti ili wapiga kura wawapime na kuchagua mmoja kati yao. Kimsingi hiyo ndiyo dhana kuu katika uchaguzi, lakini mifumo ya siasa inatofautiana ni kwa kiwango gani mgombea anaweza kutofautiana na kile kilichopo.

Wakati taarifa ya UN inaonyesha kuwa uhakika wa uhuru wa kujieleza na kufungamana kisiasa nchini umepungua, jambo hilo Waziri hakukanusha, akisema tu kuwa kiwango cha uhuru kilichopo kwa jumla kinaridhisha.

Anatoa maelezo kuwa kuna wagombea 17 wa nafasi ya urais, hakusema kuwa imepita muda wa miaka minne na nusu hakuna shughuli za wazi za siasa na vikao vya bunge kuonekana kwa njia ya mtandao na televisheni ni kwa nadra.

Hilo ni eneo mojawapo ambalo wasimamizi wa uchaguzi huwa wanaliangalia, yaani usawa katika maandalizi ya uchaguzi mkuu na pia usawa wa kampeni, kuhesabu kura.

Ila ziko kanuni kadhaa na mazoea hasa katika dhana nzima ya uangalizi wa kura ambazo zinamsaidia Waziri Kabudi, na kwa jumla inatazamiwa kuwa waangalizi kutoka nje hasa wanaotoka Umoja wa Ulaya wanaweza kuuliza hapa na pale kuhusu usimamizi na uendeshaji wa uchaguzi mkuu, bila suala la ziada.

Siyo rahisi kwa waangalizi kufikia mahali wakasema uchaguzi haukuwa huru na haki, ingawa hali hiyo ilijitokeza mwisho wa 2017 wakati Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ilipofanya uchaguzi mkuu.

Ulimuibua Felix Tshisekedi wa chama cha upinzani kilicho karibu na utawala wakati huo, kuwa ndiye aliyeshinda.

Endapo kutangazwa kwa matokeo hasa ya uchaguzi wa rais hakusababishi maandamano na vurugu, siyo rahisi kutumia vigezo vya kitaaluma na kimikataba ile ya Umoja wa Mataifa ya uendeshaji wa shughuli za siasa na kufanyika uchaguzi mkuu kuhoji matokeo.

Hata kama tuhuma zipo kuhusu kukandamizwa au kuzuiwa kwa wapinzani na hasa wagombea maridhawa wa upinzani kwa nafasi ya ubunge kama ilivyo sasa, changamoto hiyo kwa kanuni za kimataifa kwa maana ya mweleko wa kidiplomasia haziwezi kuleta kutoelewana kati ya nchi na waangalizi nje.

Inawezekana kusema kuwa jibu la Waziri Kabudi lilikuwa kwa upande mmoja linaonyesha hisia kuwa hata hivyo serikali imefanya kazi nzuri katika maeneo muhimu ya utawala bora na kuwa malalamiko ya sasa iwe ni mashirika ya UN au vikundi hapa nchini hayawezi kuvuruga msingi huo.

Anasema mwaka 2015 serikali ilikuwa inashutumiwa kwa rushwa kuenea kote nchini na ubadhirifu wa fedha za umma na hivi sasa hakuna tena lawama kama hizo, hali inayoonyesha kuwa serikali imefanya kazi kubwa. Anaeleza kuwa wafuatiliaji suala la haki za binadamu wameelekea kwingine, hisia ambayo ilitoa picha kuwa Waziri anatuhumu kuwa wachunguzi hao walikuwa wanatafuta mahali pa kuweka lawama. Hata hivyo hakusema hakuna tatizo lolote ila akauliza iwapo kuna eneo lolote duniani ambalo halina changamoto hizo.

Kusema kuwa changamoto za haki za binadamu zipo kila mahali ni kama kujibu kuwa siyo tatizo na wakati huo huo kukiri kuwa tatizo lipo. Suala la umuhimu wa tatizo hilo katika uchaguzi mkuu hata hivyo ni gumu kwani mazingira ya kupungua kwa uhuru wa kisiasa pia ni ya ushabiki wa kisiasa, kuwa katika nchi ambako serikali inatukuzwa na wanakuwa na kila sababu ya kufanya hivyo siyo rahisi upinzani kufanya kazi, kwani unaonekana kufitinisha watu na utawala bila sababu ya msingi.

Ila utawala wenye upungufu ya wazi unarahisisha demokrasia kwani wananchi wanaielewa zaidi hisia hiyo, hata kuiamini.

Tatizo linakuja pale utawala wenye upungufu wa wazi unakataa pia demokrasia, kwa mfano pale kutaka kuongeza mihula ya kuchaguliwa kutoka miwili kuwa mitatu, kama ilivyokuwa DRC na halafu Burundi, au kutokuwepo mihula kabisa kama Uganda.

Hata hivyo, unakuta katika maeneo yote hayo ipo misingi ya kushindwa kuendesha siasa za kawaida za vyama vingi kwa kuhofia nchi kuparaganyika, kutokana na utii wa kisiasa kwa muda mrefu kuwa mikononi mwa mtu mmoja na chama kimoja.

Inabidi yeye mwenyewe atake kuwe na mabadiliko na ahamishie utii wake kwa huyo atakayechaguliwa, kwani nje ya hapo siasa inakuwa ni jitihada ya kumwondoa, kwa wingi wa kura za hapana, rais asiyetaka kuondoka lakini pia siyo rahisi.

# KINAMAMA MPOO...

## ▪Kumbe kibwagizo, si dalili 50/50
## ▪Hutumiwa kushangilia kinababa



Halima Mdee, mwanamke wa kwanza mbunge mpinzani mkoani Dar es Salaam, ni mwakilishi wa jimbo la Kawe-CHADEMA. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAKATI kampeni za uchaguzi mkuu zinapamba moto na wanawake waking'ara majukwaani kushangilia na kupigia wagombea wanaume vigelegele, sehemu kubwa ya jamii inaendelea kuwaangalia kwa dhana tofauti, ikiamini kuwa hawajaiva kushika uongozi.

Na wakati mwingine huwatolea hukumu na kuonekana kama viumbe wasioweza kuleta mabadiliko katika jamii.

Jambo hilo ni kinyume na mitizamo ya kimaendeleo na kidini inayosisitiza nafasi ya mwanamke katika uongozi.

Licha ya dhamira ya serikali kutaka kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi kwa asilimia 50 kwa 50 hali halisi inaonyesha kuwa bado wanawake wako nyuma katika nafasi hizo.

**TATIZO NI NINI?**

Zipo sababu nyingi zenye kumkwamisha mwanamke katika nafasi za uongozi na moja kati ya vikwazo vyake ni mfumo dume ndani ya vyama vya siasa.

Imebainika kwamba vyama vingi vya siasa vinawatumia wanawake katika kuhamasisha na kuongeza idadi ya wanachama na kueneza sera za chama lakini si kuwapa uongozi .

Nyakati kama hizi za kampeni kuelekea uchaguzi mkuu vyama vya siasa vimekua vikiwatumia wanawake kuwavuta wapigakura lakini havimuoni kama ni mdau wa nafasi ya uongozi na kufanya maamuzi.

Mwenyekiti wa kamati ya amani na viongozi wa dini Tanzania, Salum Hadi, wakati akizungumza katika mkutano unaojadili nafasi ya mwanamke kuelekea uchaguzi mkuu, anasema:

"Nguvu ndogo ya mwanamke kiuchumi, rushwa, lugha za kudhalilisha, mila potofu na ubaguzi wa kijinsia husababisha baadhi ya wanawake washindwe kujiamini katika kukabiliana na vitendo mbalimbali vya ukatili wa kijinsia."

Anasema wanawake wana nguvu na uwezo katika uongozi hivyo wapewe nafasi kwa kuwachagua kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

"Tunaamini wazi wanawake wakichaguliwa kushika nafasi za uongozi wataendeleza vita ya rushwa, ufisadi, dawa za kulevya na mengine mengi kwa ustawi wa taifa letu ikiwa ni pamoja na kusimamia haki za wanyonge."anakumbusha .

Anaeleza kuwa kamati ya amani na viongozi wa dini inasisitiza umuhimu wa nafasi ya mwanamke katika uongozi ambapo wana mchango mkubwa katika kuinua uchumi.

**NI WANAMAPINDUZI**

Aidha, anasema wanawake wakichaguliwa katika nafasi za uongozi watatunga sheria na kushiriki katika vyombo vya uamuzi hivyo maendeleo na mapinduzi makubwa ya kiuchumi katika taifa yatatokea.

"Wanawake ni zaidi ya nusu ya idadi ya watu duniani hivyo ili kutokomeza umasikini ni lazima wapewe nafasi na kushirikishwa kikamilifu katika uongozi."

"Biblia inasema wanawake watangazao habari ni jeshi kubwa Zaburi 68:11 hivyo ni wazi wanayo nguvu ya kukamilisha hili".

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tamwa), Rose Reuben, anasema ushiriki wa wanawake katika siasa na katika ngazi za maamuzi ni eneo lililo na changamoto lukuki na hivyo linahitaji kuhimizwa na viongozi wa ngazi za juu,asasi za kiraia,wanawakke wenyewe na viongozi wa dini.

Anaeleza kuwa takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 37 ya wanawake iliyoko katika ngazi za maamuzi na kuna mapengo katika ushiriki wao ambayo hayana budi kuzibwa.

Anasema mapengo hayo ni pamoja na lugha za kudhalilisha wakati wa uchaguzi zinazowakatisha tamaa wanawake kuwania nafasi za uongozi, uteuzi usiozingatia jinsia ndani ya vyama vya siasa, hofu na kutojiamini kwa baadhi ya wanawake wanaogombea na ilani za vyama zisizozingatia jinsia.

"Mapengo mengine yaliyobainika ni rushwa ya ngono ambayo hutumika wakati wa uchaguzi, rushwa ya fedha, uchumi duni kwa wanawake wanaotaka kugombea na hivyo hupelekea kushindwa kufanya kampeni.

> Wanawake wanao umuhimu mkubwa wa kupewa nafasi ya kushiriki katika ngazi za maamuzi ili kutetea maslahi na mahitaji ya wanawake wengine katika nyanja mbalimbali," anasema.

Anaeleza kuwa viongozi wa dini wana nafasi kubwa katika kuhimiza jamii kuondoa mila na mitazamo potofu inayochochea ushiriki duni wa wanawake katika siasa na katika ngazi za uamuzi.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar Dk. Mzuri Issa Ali, anasisitiza kuwa nafasi ya mwanamke katika uongozi ni muhimu katika uimarishaji wa maendeleo ya wanawake na uchumi nchini.

"Wanawake wanao umuhimu mkubwa wa kupewa nafasi ya kushiriki katika ngazi za maamuzi ili kutetea maslahi na mahitaji ya wanawake wengine katika nyanja mbalimbali," anasema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Zanzibar, Profesa Issa Haji Ziddy, anasema dini hazijamkataza mwanamke kuwa kiongozi.

"Mwanamke hajakatazwa kushiriki katika vyombo vya kutoa uamuzi ila tu ameelekezwa kufuata taratibu na misingi ya dini ili uongozi wake uwe halali na haki," alisema.

Anasema kuwa dini imeweka bayana kwamba mwanamke anawajibu wa kufanya kazi za halali ikiwemo kushika nafasi za uongozi kama mwanamume pasipo kuwapo kwa ubaguzi wa aina yoyote.

Aidha, anaongeza kuwa viongozi wa dini wana dhamana ya kuwasimamia wanawake katika uongozi ili wasikiuke maadili.

Sheikh Said Abdallah Mohamed, kutoka ofisi ya Mufti Pemba, anasema ipo haja ya kuandaliwa kwa mkakati maalum unaolenga kumuandaa mtoto wa kike kushika nafasi za uongozi kwa kuzingatia maadili na maelekezo ya dini.

"Viongozi wa dini tunawajibu wa kuandaa mkakati wa kumwezesha mtoto wa kike kushika nafasi ya uongozi katika jamii bila kukiuka maadili na miiko," anasema.

Mgombea urais wa Tanzania kupitia chama cha ADC Queen Sendiga, akizungumza katika kusanyiko hilo, anasema usawa wa kijinsia uliopo ndani ya chama chake umemwezesha kugombea nafasi hiyo ya juu ambayo ni kwa mara ya kwanza kusimamisha mgombea mwanamke.

Anasema wanawake wanaweza kuwa viongozi katika nafasi za juu na si jambo jema kuwaachia wanaume pekee nafasi hizo.

Mgombea huyo anawataka wanawake kumuunga mkono na kumpigia kura bila ya kuangalia vyama vyao vya siasa ili wanawake kuiongoza serikali na kwamba uwezo huo anao.

Aidha, anazitaka asasi mbali mbali za utetezi wa wanawake kumuunga mkono kwa sababu lengo lake ni kuhakikisha sauti za wanawake zinafikiwa na makundi yoye kwa ajili ya kufikisha kilio chao kinachotokana na changamoto zinazowakabili.

"Masikitiko yangu makubwa hakuna taasisi za wanawake zilizojitokeza kuniunga mkono katika kipindi chote tangu nilipochukua fomu za urais na baadaye kupitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)"anasema.

Anaeleza kuwa endapo atapata ridhaa ya kuchaguliwa atahakikisha anatengeneza usawa wa kidemokrasia na upatikanaji wa haki za binadamu na maslahi bora kwa wanawake na Watanzania wote.

SALOME MAKAMBA:

# "Kubezwa kisa ni viti maalumu kumenisukuma ubunge kamili"


Solome Makamba, katika mahojiano na mwanahabari Maduhu. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

JIMBO la Shinyanga Mjini tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi miaka 28 sasa, halijawahi kuona mwanamke akipitishwa na chama chochote kugombea ubunge.

Lakini mwaka huu mambo ni tofauti, kwa mara ya kwanza mwanamke amepenya kugombea ubunge Shinyanga Mjini, akichuana na wanaume kadhaa.

Ni Salome Makamba, ndiye mwanamke wa shoka aliyeshinda vita dhidi ya mfumo dume na kupitishwa na CHADEMA kupeperusha bendera yake Shinyanga Mjini.

Katika kura za maoni ndani ya chama hicho, aliwabwaga wanaume sita waliokuwa wapinzani wake.

Anakipongeza chama chake kwa kumwamini na kumpitisha kugombea ubunge na kuweka historia ya mwanamke wa kwanza kugombea ubunge katika jimbo hilo tangu mfumo wa vyama vingi ulipoanzishwa nchini 1992, na sasa amevunja mwiko.

Salome anasema katika safari yake ya kisiasa mwaka 2010, alijiunga na CHADEMA na uchaguzi mkuu wa 2015 aliteuliwa kuwa mbunge wa viti maalum mkoani Shinyanga.

**KUBEZWA KUMEMSUKUMA**

Akieleza sababu ya kugombea ubunge anasema kuwa kubezwa kumechangia. Anasema pamoja na nia ya kupitisha na kufikisha hoja za kutetea wananchi wa Shinyanga kwa nguvu alipokuwa viti maalumu, hoja hizo zilikuwa zinakosa nguvu kwa vile hakuna aliyemuunga mkono kisa ni wa viti maalumu na kulazimishwa kukaa chini kila akizungumza.

Aidha, anasema kila akitoa hoja alikuwa haungwi mkono na wabunge wengine wa mkoa huo.

"Nilikuwa mbunge wa viti maalum mkoani Shinyanga kwa miaka mitano. Lakini nilipokuwa ndani ya bunge na nilipopenyeza hoja za kutetea wana Shinyanga zilikosa kuungwa mkono kutoka kwa wabunge kwa sababu tu kaitoa mbunge wa viti maalum," anasema Salome.

"Nilikuwa nashangaa naambiwa kaa chini, mbunge husika wa jimbo hilo yupo mbona hajazungumzia tatizo hilo, na akipewa nafasi kuzungumza ana anza kunishambulia bungeni na kuitetea serikali, wakati wananchi wanaumia badala ya kuishauri serikali nini cha kufanya sababu hiyo ndiyo kazi ya wabunge,"anaongeza.

Anasema baada ya kuona hoja zake zinabezwa za kutetea wananchi wa Shinyanga sababu ya viti maalum, ndipo akaona ni vyema agombee jimbo mahali ambapo ni nyumbani kwao na huo ndiyo mwanzo wa kujitosa.

"Mimi ni mwanamke ninayejiamini na nilianza kuwa kiongozi tangu nikiwa kidato cha tano Sekondari ya Wasichana Koaki iliyopo Tarime, hivyo naweza kuwatumikia wana Shinyanga na kuwaletea maendeleo. Na ninaomba waniamini wanipe nafasi, na waachane kabisa na masuala ya mfumo dume, kwani wanawake tunaweza kuwa viongozi," anasisitiza.

**ANACHOLENGA**

"Kazi ya mbunge ni kuishauri serikali ili iwajibike kwa wananchi, jambo ambalo kwangu ni kitu kidogo kwa sababu nazijua shida za wananchi wa Shinyanga na nini wanakitaka. Nitapeleka hoja zangu ili kufanyiwa kazi kwa sababu sitakuwa tena mbunge viti maalum bali ni mbunge kamili,"anaeleza.

Aidha, anasema alifanikiwa kupenya kugombea nafasi hiyo mara baada ya kuona utendaji wake wa kazi ni mkubwa. Na ni mwanamke jasiri katika utetezi wa hoja za wananchi.

"Kabla ya Bunge la 11 kuvunjwa, Watanzania na wananchi wa Shinyanga waliniona bungeni kupitia vyombo vya habari, namna nilivyokuwa nikipigania maslahi ya wachimbaji wadogo wa almasi mgodi wa Maganzo, ambao wanapewa mchanga wa marudio na mgodi wa Williamson Diamond, huo ni mfano tosha wanawake tunaweza kuchapa kazi,

"Pia maendeleo yote mnayoyaona katika majimbo yote sita ya Shinyanga na mimi mchango wangu upo, sababu kazi ya mbunge ni kusemea matatizo ya wananchi kwa serikali ili itekeleze, hakuna mbunge ambaye ataleta maendeleo kwa kutumia fedha zake mfukoni huo ni uongo, hivyo naomba wana Shinyanga wanipe nafasi,"anasema Makamba.

Joseph Ndatala ni Katibu wa CHADEMA Wilaya ya Shinyanga Mjini, anasema, chama kinaamini uwezo wa kila mtu katika utendaji kazi bila ya kubagua jinsi ya mtu ndiyo maana kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu kimepitisha wagombea wengi wanawake.

Anasema suala la mfumo dume lilishapitwa na wakati na wanawake nao wana haki sawa na katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi na yule ambaye atashinda kwenye kura za maoni ndiye atatangazwa bila ya kujali jinsi yake.

"CHADEMA tunaamini katika uwezo wa kila mmoja kufanya kazi bila ya kujali jinsi yake na ukiangalia katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu wanawake waliotiania ya ubunge wengi wamepita kugombea nafasi hizo, sababu ya kuonyesha uwezo wao mkubwa wa kuchapa kazi na nia ya kuwatumikia wananchi," anasema Ndatala.

"Uchaguzi mkuu wa mwaka huu tumeweka historia kwenye Jimbo la Shinyanga Mjini, kupitisha mgombea mwanamama kupeperusha bendera ya CHADEMA kugombea nafasi ya ubunge, kitendo ambacho hakijawahi kutokea mjini hapa, kuwa na mgombea ubunge mwanamke kushindana na wanaume," anaongeza.

Pia, anawataka wananchi Shinyanga kumpima mgombea huyo mwanamama katika utoaji wa sera kwenye kampeni zake, na siyo kumhukumu kwa jinsi yake na kunyima fursa ya uongozi, sababu ya kuendekeza masuala ya mfumo dume ambao ulishapitwa na wakati

Mzee wa kimila Ngassa Maganga, mkazi wa Mwamala, wilayani Shinyanga, mkoani hapa, anaelezea mila na desturi jinsi zinavyomkandamiza mwanamke na kunyima fursa ya kuwa kiongozi kwenye uchaguzi mbalimbali.

Anasema mila na desturi za Wasukuma, zinamtambua mwanamke kama malalamikaji na siyo kutoa uamuzi, hivyo akiwa kiongozi ataonekana amedharau wanaume ndiyo maana huwa ni vigumu kushinda nafasi za uongozi, na kuambulia viti maalumu ili aendelee kuwa chini ya mwanaume.

"Mila na desturi hazimpatii nafasi mwanamke kuwa na sauti ndani ya jamii anaonekana kama mtu wa kulalamika ambaye kazi yake ni kupokea maagizo kutoka kwa wanaume na siyo kutoa uamuzi. Ndiyo maana jamii inaamini kuwa akiwa kiongozi atakuwa amevunja miiko ya mila na desturi," Maganga, anasema.

Mkoani Shinyanga kuna majimbo sita ya uchaguzi, ambayo ni Ushetu, Msalala, Kahama Mji, Kishapu, Solwa, na Shinyanga Mjini, na katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, wagombea wote katika majimbo matano ni wanaume kasoro hilo la Shinyanga Mjini.

Upungufu huo unaonyesha kuwa kunakosekana uwiano wa usawa wa kijinsia.

Katika jimbo la Shinyanga mjini napo wagombea wa nafasi ya ubunge kwenye vyama vingine wamepitishwa wote wanaume, tofauti na chama hicho cha CHADEMA, ambapo Salome atakuwa akipambana na wanaume kwenye kampeni.

Mwanaharakati kutoka Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP) Ananelia Nkya, ambaye pia ni mwanahabari mbobezi, anasema suala la usawa wa kijinsia kwenye nafasi za uongozi Tanzania bado ni changamoto.

Anasema jitihada za makusudi zinahitajika ili kuondoa mifumo ya kuona wanawake hawawezi kuwa viongozi bora.

Anasema bado inahitajika elimu kwa wananchi ili kuwatambua wanawake kuwa ni viongozi wazuri, pamoja na kinamama nao kujitambua kuwa wanaweza na wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi ili kufikia malengo ya usawa wa kijinsia ya uwakilishi wa 50 kwa 50 katika nafasi za uongozi na maamuzi.

"Wanawake ni wachache kwenye nafasi za uongozi, mfano Bunge la 11, wabunge walikuwa 393, wanawake ni asilimia 36.8, wakuchaguliwa majimboni ni asilimia 25...," anasema Dk. Nkya.

Pia anatoa wito kwa wanawake waendelee kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uongozi kwenye uchaguzi ujao wa serikali za mitaa mwaka wa 2024 na mkuu wa 2025.

# THOMAS ISIDORE NOËL SANKARA

- Rais 'Malaika' aliyeongoza Afrika
- Alijenga nchi bila fedha ya 'beberu'
- Kifo chake chabaki utata hadi leo



Mwanapinduzi Thomas Sankara, enzi za uhai wake. Licha ya kuleta mapinduzi aliuawa ndani ya miaka minne ya urais. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

UNAPOSOMA au kusimuliwa habari za kiongozi huyu wa Afrika wazo ambalo litakujia ghafla ni hili: "Kwanini aliuawa?" "Aliyemuua hakujua wala kuona haya?"

Huyo ni Thomas Sankara almaarufu " Che Guevara wa Afrika", anayebakia kuwa shujaa kwa Waafrika wengi.

Sankara alichukua uongozi wa Upper Volta 1983 akiwa na miaka 33, na lengo lake lilikuwa kuondoa ufisadi, rushwa na ubeberu wa Kifaransa na kwa kuanzia bila kufanya ajizi, alibadilisha jina la nchi hiyo la Upper Volta na kuita nchi hiyo Burkina Faso au ardhi ya watu waadilifu ("Land of Upright Man").

Kiongozi huyo wa Burkina Faso, aliyekuwa na itikadi za mrengo wa kushoto (ukomunist) licha ya kutaka kulifikia taifa lake kwenye usawa, udugu na lenye kuheshimu demokrasia alidaiwa kuuliwa na jenerali wa jeshi.

**ALITISHIA KWA MAKUBWA**

Mosi, alitumia rasilimali za taifa hilo bila kuomba msaada wa wageni kujenga barabara na reli zilizounganisha majimbo mbalimbali ya Burkna Faso.

Hakutaka magari ya bei mbaya aliuza msururu wa benzi za serikali na kutangaza gari la Renault 5 ambalo lilikuwa la bei ndogo wakati huo kuwa ndilo linalotumiwa na viongozi wa serikali wote bila kujali vyeo. Bei yake leo ni Shilingi milioni 11 . (sawa na dola 4,694.15)

Ndani ya wiki moja Sankara aliwachanja chanjo ya homa ya manjano, surua na uti wa mgongo watoto zaidi ya milioni 2.5 wa nchi hiyo kuokoa maisha yao.

Alianzisha kampeni ya kitaifa ya kufuta ujinga na kuongeza idadi kubwa ya watu wanaofahamu kusoma na kuandika kutoka asilimia 13 mwaka 1983 hadi asilimia 73 mwaka 1987.

Alikuwa mwanamazingira aliyepanda miti zaidi ya milioni 10 kukabiliana na ongezeko la jangwa nchini Burkina Faso.

Alitokomeza ukeketaji, ndoa za utoto na hata za kulazimishwa, kukataza wanaume kuoa wake wengi. Aidha aliwapa wanawake wenye uwezo nafasi za juu serikalini huku akiwahamasisha kufanyakazi na pia aliwaingiza kwa wingi jeshini.

Alishusha mshahara wa watumishi wa umma na wa kwake na kuachana na kutumia tiketi za daraja la kwanza anaposafiri kwa ndege. Alisimamia kilimo na kuhakikisha nchi hiyo inajitosheleza kwa chakula.

> Alianzisha kampeni ya kitaifa ya kufuta ujinga na kuongeza idadi kubwa ya watu wanaofahamu kusoma na kuandika kutoka asilimia 13 mwaka 1983 hadi asilimia 73 mwaka 1987.

**KUPINGA UBEBERU**

Ni shujaa aliyewaambia viongozi wa Afrika kwenye moja ya Mkutano wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) kuwa hataki misaada ya mabeberu kwa imani kuwa anayekulisha na kukutana anakudhibiti "he who feeds you, controls you."

Jijini Ouagadougou, Sankara aliligeuza ghala la chakula la jeshi kuwa 'supermarket' kwa ajili ya watu wote na akawahimiza wafanyakazi wa serikali kutoa mshahara wao wa mwezi kwa ajili ya projekiti za serikali.

Alikuwa anaendesha gari lake mwenyewe na kukataa picha yake isitundikwe ukutani kwenye ofisi za serikali na popote kwingine. Alipoulizwa alijibu kuna sankara wengine zaidi ya 7,000,000 picha zao ziko wapi?

Alikataa kutumia viyoyozi 'air conditioning' kwa maelezo kuwa mamilioni ya Waburkinabee hawana viyoyozi kwanini yeye? Aidha, alishusha mshahara wake na kuwa Dola 450 sawa na Sh. 1,000,000 leo.

Shujaa huyo wa Afrika alibadilisha jina la nchi yake na kuiita Burkina Faso, kutoka jina la kikoloni la Upper Volta. Kabla ya kuingia kwenye siasa alikuwa kapteni wa jeshi la Burkina Faso.

Alikuwa makini kisiasa akifuata mrengo wa kimapinduzi wa itikadi ya Kikomunisti wa 'Marxist' aliyeliongoza taifa lake kwa miaka minne kuanzia mwaka 1983 hadi 1987.

Aliheshimika na kuonekana kama rais mwenye kipaji 'karisma' na mwanamapinduzi halisi wa Afrika akiitwa "Che Guevara wa Afrika".

**KUULIWA**

Akiwa amezaliwa Desemba 21, 1949, katika mji wa Yako, wakati huo, Burkina Faso ikiitwa Upper Volta, Sankara aliuawa Oktoba 15, 1987 jijini Ouagadougou na majenerali wa jeshi, baada ya kushika uongozi wa taifa hilo kuanzia mwaka 1983.

Sankara aliuawa na kiongozi wa mapinduzi yaliyodumu kwa muda mfupi nchini Burkina Faso, si muuaji kutajwa kuwa ni Jenerali Gilbert Diendere.

Jenerali huyo ameshtakiwa kwa kuhusika katika mauaji ya Sankara aliyeuawa mwaka 1987 na sasa ametimia miaka 33 baada ya mauaji hayo.

Jenerali Gilbert Diendere anatajwa kuwa ofisa wa ngazi ya juu zaidi kushtakiwa kwa mauaji hayo.

Rais Sankara.

Rais huyo aliuawa na kundi la askari, lakini hadi sasa mazingira halisi ya kifo chake yanaelezwa kuwa yanasalia kuwa jambo lenye utata.

**MRITHI WA SANKARA**

Baada ya kifo cha Sankara, Rais Blaise Compaore alikuwa mrithi wake akisalia madarakani kwa miaka 27.

Serikali ya mpito, iliyochukua mamlaka baada ya kung'olewa madarakani kwa Compaore mwaka 2014, iliahidi kuchunguza mauaji hayo upya.

Uchunguzi huo ulisababisha maofisa wengine 10 wakashtakiwa kuhusiana na mauaji ya Sankara.

Jenerali Diendere ambaye ambaye anakabiliwa na mashtaka kuhusiana na mapinduzi yaliyofanyika Oktoba 7, 1987 na kufunga ukurasa wa maisha ya Sankara.

Licha ya Jenerali Diendere, kudaiwa kuhusika na mauaji ya Sankara aliendelea kuwa mkuu wa ujasusi katika utawala wa Compaore.

Aidha, licha ya kuchukuliwa kama muuaji anadaiwa alikuwa rafiki wa karibu na mshirika mkuu wa kisiasa wa Sankara kabla ya kifo chake.

Wakati wa utawala wa Rais Compaore uchunguzi uliofanyika kuhusiana na mauaji hayo ulikuwa wa mafanikio kidogo na kuongeza maswali.

**ALIPIGWA RISASI KILA MAHALI**

Matokeo ya ukaguzi wa kimatibabu uliofanywa kwenye mabaki ya mwili wa Thomas Sankara miaka 28 baada ya kuuawa, yalionyesha kuwa mwili wake ulijaa risasi .

Kwa mujibu wa wakili aliyekuwa akiwakilisha familia alipigwa risasi kila mahali na taarifa kuripotiwa kwenye ukurasa wa Facebook wa kituo cha habari cha Burkina 24. Hayo yalitokea mwaka 2015

familia yake ilikuwa ikisubiri matokeo ya DNA kuthibitisha kwamba mabaki hayo yalikuwa ya Sankara, wakili Benewende Sankara aliviambia vyombo vya habari nchini humo.

Sankara aliuawa katika mazingira ya kutatanisha akiwa na umri wa miaka 37 na kundi la wanajeshi Oktoba 1987 na alizikwa kwa haraka kufuatia mapindupi yaliyoongozwa na mrithi wake Blaise Compaore.

> familia yake ilikuwa ikisubiri matokeo ya DNA kuthibitisha kwamba mabaki hayo yalikuwa ya Sankara, wakili Benewende Sankara aliviambia vyombo vya habari nchini humo.





# Zabuni bomba la mafuta kutangazwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU chache baada ya serikali za Tanzania na Uganda kukubaliana juu ya ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima hadi Chongoleani, Tanga, Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) limesema litatangaza upya zabuni ya utekelezaji wa mradi huo.

Akizungumza jana jijini hapa na kituo kimoja cha runinga nchini, Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, Dk. James Mataragio, alisema kuna vikwazo vilijitokeza baada ya mradi kusimamishwa ambapo kuna kampuni zilikuwa tayari zimeshinda zabuni na zilikuwa kwenye hatua ya kukamilisha mchakato wa manunuzi.

"Sasa baada ya hatua ile ya kusimamisha mradi mambo yakabadilika hapo katikati ikaja corona, kwa hiyo zile gharama zikabadilika kitakachotokea sasa hivi ni kwamba ile tender (zabuni) itatangazwa tena," alisema.

**Sasa baada ya hatua ile ya kusimamisha mradi mambo yakabadilika hapo katikati ikaja corona, kwa hiyo zile gharama zikabadilika kitakachotokea sasa hivi ni kwamba ile tender (zabuni) itatangazwa tena.**

Alibainisha kuwa kampuni zilizokuwa zimeomba zitarekebisha vitu mbalimbali kutokana na gharama nyingine zimependa na kushuka, na hivyo hatua hiyo itachelewesha kidogo mchakato wa manunuzi.

Hata hivyo, alisema kutokana na mkataba huo wa awali kusainiwa kuna mkataba hodhi ambao utasainiwa na wawekezaji na kuna mikataba mingine midogo midogo ambayo itakamilishwa Desemba mwaka huu.

"Mikataba yote ikishakuwa tayari sasa uamuzi wa kuwekeza kwenye mradi unatolewa na tunaanza kutafuta fedha za kuanza mradi, kwa upande wa Tanzania TPDC sisi tunakuwa ni wana hisa tutamiliki hisa katika Kampuni ya ECOP kwa niaba ya serikali," alisema.

Aliongeza: "Faida tumeshaongelea nyingi za mradi, lakini kuna faida zimegawanyika katika maeneo matatu, kuna faida zitatokana na shughuli za ujenzi wa bomba kama vile ajira, utwaaji wa maeneo, kampuni zetu zitapata kazi kusafirisha mabomba ujenzi, tunategemea kutakuwa na ajira 10,000 kwa kipindi hicho."

Pia, alisema kuna faida zitatokana na uendeshaji ambapo watu 10,000 wataajiriwa ambao watatengeneza fursa kwa watu wengine 70,000 nao watanufaika na serikali itapata mapato moja kwa moja.

Alieleza kuwa ujenzi huo unatarajiwa kuanza mwaka ujao (2021) kulingana na ratiba itachukua miaka mitatu kukamilika.

"Ukianza mwakani mwanzoni utachukua miaka mitatu kukamilika," alisema.

Kuhusu fidia kwa wananchi wanaopitiwa na bomba hilo, alisema kuna kazi inaendelea kwa sasa ni kulipa fidia wananchi hao.

"Kuna maeneo ya aina mbili kuna ya kipaumbele zitakuwa zinajengwa kambi za kutengeneza mabomba na yapo maeneo 14, sasa hivi tupo kwenye hatua za kuhakikisha kwamba wale watakaopisha mradi katika hayo maeneo wanafidiwa, vile vile wale watakaopisha mradi kwenye eneo la Mkuza lote wanafidiwa," alisema.

Septemba 13, mwaka huu, Rais John Magufuli na Rais wa Uganda Yoweri Museveni walishuhudia utiaji wa saini makubaliano ya kukamilisha majadiliano ya utekelezaji wa mradi huo.

Pia, marais hao walitia saini waraka wa pamoja wa kuagiza kuanza haraka utekelezaji wa mradi huo ambao bomba litakalojengwa litakuwa na urefu wa kilometa 1,445 na kwa Tanzania litapita kwenye mikoa nane na vijiji 280 nchini.

Bomba hilo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kupitisha mapipa 216,000 kwa siku na kwa miaka 25 ya mradi huo, Tanzania itapata mapato kiasi cha Sh. trilioni 7.5.

# Askofu ahamasisha maombi ya uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Agape Santuary Ng'ong'ona jijini Dodoma, Joshua Mnyamazi, amewaomba Watanzania kujikita katika maombi ili uchaguzi mkuu 2020 ufanyike kwa haki na amani.

Askofu huyo alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa maombi ya kuombea uchaguzi mkuu ambayo yaliambatana na ibada maalumu ya ufunguzi wa mlima wa maombi.

Alisema kuwa Watanzania wanatakiwa kuweka ushabiki pembeni na kuiombea nchi ili uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu upite salama.

"Tuweke ushabiki pembeni, nawaomba tumtangulize Mungu mbele ili uchaguzi wetu uwe wa haki na amani na tunataka mema juu ya nchi yetu, bwana ahusike na uchaguzi mkuu huu," alisema.

Aidha, alisema kila Mtanzania ana wajibu wa kuomba kuhusiana na kile anachokipenda na kuacha utaratibu wa kufanya maombi Jumapili peke yake.

Katika hatua nyingine, Askofu huyo aliwataka Watanzania kuwachagua viongozi wenye sera nzuri na kuachana na wenye matusi kwani kila mmoja anataka maendeleo kwa ajili ya nchi.

"Chagueni wenye sera nzuri sio wale wenye kutoa matusi, chagueni wale wenye kumwogopa Mungu na ambao watatufanyia kitu au ambao tayari wametufanyia kitu," alisema.

Kwa upande wake, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Utatu Tanzania, Dk. Kuwayawanya Kuwayawanya, aliwataka Watanzania kutofanya makosa ya kuwachagua wagombea wasiokuwa na sera zenye misimamo ya maendeleo.

Alisema watu wanapenda kuona Tanzania inasonga mbele kimaendeleo na ndiyo maana walio wengi wanatumia muda mwingi kumuomba Mungu ili wapatikane viongozi madhubuti na wenye kujitambua.



Naibu Mwenyekiti wa Kanisa la Angalikana Sinodi ya Dayosisi ya Morogoro, Mch. Elias Chamwenye (wa pili kulia), akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa elimu ya watu wazima, iliyofadhiliwa na Chama cha Biblia Tanzania kwa kushirikiana na serikali ya Finland katika kijiji cha Magubike, Wilaya ya Kilosa juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ujerumani yaihakikishia Tanzania ushirikiano zaidi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Ushirikiano wa Ubalozi wa Ujerumani nchini, Dk. Kartin Bornemann, amesema nchi hiyo itaendelea kushirikiana na Tanzania ili ifikie malengo ya maendeleo ya nchi.

Mkuu huyo aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akitambulisha timu mpya ya ushirikiano wa maendeleo kutoka Ubalozi wa Ujerumani ambayo imewasili nchini baada ya iliyokuwapo kumaliza muda wake.

Alisema Ujerumani ilianza kushirikiana na Tanzania kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo tangu mwaka 1961, ambapo hadi mwaka 2012 imechangia jumla ya Euro milioni 229 kwa ajili ya kuendesha miradi hiyo.

"Ujerumani inafadhili miradi mbalimbali ya maendeleo kupitia GIZ na KfW, ambayo ni katika sekta ya maji, miundombinu, umeme wa jua (solar), maliasili, miradi katika mbuga za wanyama na kilimo," alisema.

Alitaja miradi mingine kuwa ni miundombinu ya makazi ya wakimbizi mkoani Kigoma, kutunza maliasili na miundombinu yake, miundombinu ya utawala bora wa fedha, kuunda nafasi za kazi kupitia mafunzo ya ufundi na sekta ya afya pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Binafsi ninafuraha na nilitamani kufanya kazi katika nchi nzuri Tanzania ninavutiwa nayo kwa muda mrefu nilipopata nafasi niliripoti mara moja," alisema.

Aliongeza: "Timu hii mpya ipo tayari kufanya kazi kwa mashirikiano na timu ya Tanzania kwa ukaribu ili kusaidia katika kuongeza kasi ya maendeleo, nawaomba muwe huru kutumia fursa hii vyema, sisi ni wasaidizi kwa malengo yenu, tunataka tuone kama mambo tunayowasaidia kwa maendeleo yanagusa umuhimu mliojiwekea."

Kwa upande wake, Mkuu mpya wa Ushirikiano wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye ubalozi wa Ujerumani anayehusika na masuala ya afya, Johannes Serrfechter, alisema ushirikiano kati ya pande hizo mbili, sekta ya afya imepewa kipaumbele hasa katika afya ya mama na mtoto.

Alisema katika miaka mitano iliyopita miradi yao imechangia kupunguza vifo vya mama na watoto na kwamba Ujerumani iko tayari kuendelea na ushirikiano na Tanzania ili kuboresha maisha ya Watanzania.



# TAKUKURU yabaini viashiria 52 vya rushwa

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapa imebaini viashiria 52 vya rushwa kwa waliokuwa watiania na wagombea wa uchaguzi wakati wa mchakato wa kura za maoni.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Thomas Msuta, alisema taasisi hiyo imefanya uchunguzi na kubaini vitendo vya rushwa ya fedha na vitu baada ya kupokea tuhuma za viashiria 52 kwa wilaya zote mkoani hapa.

Pia, alieleza kuwa taasisi hiyo inaendelea na uchunguzi ili kubaini tuhuma hizo na baada ya kukamilisha watuhumiwa watafikishwa kwenye sehemu husika za kutoa uamuzi.

**Katika uchunguzi huo walibaini baadhi ya wagombea kujitoa kwenye kinyang'anyiro kwa sababu ya shinikizo kutoka baadhi ya wenzao.**

"Katika kipindi hiki cha uchaguzi kuanzia mchakato wa kura za maoni, TAKUKURU tulibaini viashiria 52 vya rushwa kutoka kwa wagombea mbalimbali kuanzia ngazi ya udiwani hadi ubunge na tayari mashauri yamefunguliwa ili kuthibitisha tuhuma hizo," alisema Msuta.

Alisema katika uchunguzi huo walibaini baadhi ya wagombea kujitoa kwenye kinyang'anyiro kwa sababu ya shinikizo kutoka baadhi ya wenzao.

Hivi karibuni TAKUKURU nchini ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuwashughulikia wagombea wote ambao watabainika kutumia rushwa kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Katika taarifa hiyo ilitahadharisha kuwa wagombea wote wanapaswa kuzingatia sheria na kanuni na taratibu za nchi katika kushiriki uchaguzi kwa kuhakikisha wananchi wanawachagua viongozi wanaowahitaji kwa ushawishi wa sera na utendaji kazi wao.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, liliwataka wagombea wote kufanya kampeni za kistaarabu na kutumia lugha za staha wanapokuwa jukwaani, ili kuzuia migogoro na chuki miongoni mwa wananchi na wanasiasa.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema jeshi lake limejipanga kudhibiti vitendo vyote vya uhalifu na viashiria vya uvunjifu wa amani katika uchaguzi mkuu.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akizungumza na vikundi vya wajasiriamali wa Kata ya Isyonje, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe jana, kuhusu umuhimu wa kujiunga na vikundi ili kupata mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Taasisi kilimo zaomba benki kuondoa masharti mikopo

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

TAASISI zinazojihusisha na masuala ya kuhamasisha kilimo nchini, zimeiomba serikali kuboresha na kuondoa baadhi ya masharti yaliyowekwa na taasisi za kifedha ili kuwasaidia wakulima kukopesheka kwa urahisi.

Ofisa Masoko wa Kampuni ya Agricom kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Mwita, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu wajibu wao kuwasaidia wakulima kuwaunganisha na taasisi za kifedha.

Mwita alisema kilimo ni miongoni mwa sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa nchi kufikia uchumi wa kati na kuhakikisha mkulima anakuwa sehemu ya mafanikio hayo lazima mazingira wezeshi yaandaliwe.

Alisema miongoni mwa mambo yanayotakiwa kufanyiwa kazi ni serikali kuziangalia au kuzishauri taasisi za kifedha kuwaandalia mazingira rafiki ya ukopeshaji ili yasimuumize mkulima na aweze kurejesha kwa wakati.

"Tukiwa miongoni wa taasisi binafsi nchini tunaishauri serikali kupitia upya utaratibu wa utoaji mikopo unaofanywa na taasisi za kifedha ili kuondoa masharti yote yanayomkandamiza mkulima wakati wa urejeshaji mikopo kwa sababu wakati mwingine anaposhindwa kurejesha hulazimika mazao yake kuuzwa ili kufidia," alisema Mwita.

Aliongeza kuwa kampuni ya Agricom ambayo inahusika na uuzaji pamoja na usambazaji wa zana za kilimo imekuwa mstari wa mbele kujali hali za wakulima kwa kuhakikisha wanauza zana zao kwa bei nafuu.

Alisema kupitia maonyesho ya Nanenane, wanauza zana za kilimo ikiwamo matrekta kwa punguzo la bei, ili kila mkulima anayehitaji aweze kununua.

Baadhi ya wakulima ambao ni wanufaika wa mikopo ya benki akiwamo Julius Mwaikusa, ambaye alilalamikia baadhi ya masharti kusababisha wakose mikopo na kushindwa kutimiza malengo yao.

Alisema hitaji yao ni kupata mikopo ya zana za kilimo kama matrekta na maguta kwa ajili ya kulima, kupanda na kuvuna.

# Wakulima washauriwa kuzingatia teknolojia

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

WAKULIMA wadogo wameshauriwa kuzingatia matumizi ya teknolojia bora za kilimo na kuachana na kilimo cha mazoea, ili wawe wakulima wakubwa.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa akizungumza na teknolojia mbalimbali za kilimo ambazo taasisi hiyo imebuni.

Alisema wakulima wanatakiwa wazalishe kwa kufuata utaratibu wanaoelekezwa na wataalamu wakiwamo maofisa kilimo wa vijiji pamoja na wanaouza pembejeo za kilimo.

Alisema taasisi hiyo haitaki watu kuendelea kujiita wakulima wadogo wakati teknolojia zipo nyingi na kwa sasa hivi wamekuja na teknolojia ya kupima udongo na kuwashauri wakulima mazao yanayofaa kulingana na aina ya virutubisho.

"Kwa sasa serikali imefanikiwa kuingia kwenye uchumi wa viwanda na kwamba kuna unahitaji malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda vinavyoendelea kuanzishwa, sasa tukiendelea kuwa na wakulima wadogo wengi haitatusaidia," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza kuwa maofisa kilimo wa vijiji wanatakiwa kuanzisha utaratibu wa kufuatilia ukuaji wa wakulima kwenye maeneo yao, ili kuepuka kuwa na wakulima ambao hawakui kila mwaka.

Alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kuzalisha mazao ya kimkakati kwa kutumia mbegu za kisasa zinazozalishwa na taasisi hiyo, ili wainuke badala ya kuendelea kuwa vile vile huku baadhi wakitumia mbegu za kienyeji.

Dk. Bucheyeki alisema kwa sasa taasisi hiyo imezalisha mbegu mbalimbali za kisasa ambazo wakulima wanashauriwa kuzitumia ili kuongeza tija zikiwamo za maharagwe, mahindi, alizeti, parachichi na ngano.

Mtafiti wa zao la viazi mviringo katika taasisi hiyo, Dk. Dolla Mende, alisema utafiti walioufanya wamegundua mbegu mbalimbali ambazo zikitumiwa na wakulima zitawainua kutokana na kuzaa vizuri na kukinzana na magonjwa pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema wameshazalisha aina 10 za mbegu za viazi na aina nyingine zipo kwenye hatua mbalimbali za utafiti ili kuangalia ubora wake na kama zitafaa zitasambazwa kwa wakulima ili waendelee kuzizalisha.





# Mgombea wa CCM atangazwa mshindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imemtangaza rasmi mgombea wa uwakilishi kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Haji Omar Kheir, kuwa mwakilishi mteule wa Jimbo la Tumbatu.

Msimamizi wa Uchaguzi wa ZEC Wilaya ya Kaskazini A, Miza Pandu Ali, aliwaambia waandishi wa habari katika ofisi za tume hiyo zilizoko Gamba, Kaskazini Unguja, kuwa Haji ametangazwa kuwa mshindi baada ya kuwa mgombea pekee wa nafasi ya uwakilishi kwa jimbo hilo.

Alisema tume imefanya uamuzi huo kwa mujibu wa mashart ya Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Namba 4 ya mwaka 2018 kifungu cha 59(a)(b) ambacho kinamtaka msimamizi wa uchaguzi kumtangaza mgombea pekee katika jimbo au wadi.

Aidha, tume imemtangaza Othman Khamis Fumu kuwa diwani mteule wa wadi ya Kipange na Simai Vuai Khamis kuwa diwani mteule wa wadi ya Kijini kwa tiketi ya CCM.

Akizungumza kwa niaba ya wateule wenzake, Haji alisema wagombea wote katika jimbo la Tumbatu wameridhishwa na busara na hekima kwa watendaji wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika kufanya uamuzi sahihi wa pingamizi na rufani zilizowasilishwa.

Taarifa kwa vyombo vya habari juu ya uamuzi wa rufani iliyotolewa na ZEC, tume imewaengua Haji Ali Haji, mgombea wa nafasi ya uwakikishi Jimbo la Tumbatu, Zuli Juma Simba wa Wadi ya Kijini na Salum Khamis Maliki Wadi ya Kipange wote kutoka Chama cha ACT-Wazalendo baada ya kushindwa kutimiza vigezo vya uteuzi.

**Tume imemtangaza Othman Khamis Fumu kuwa diwani mteule wa wadi ya Kipange na Simai Vuai Khamis kuwa diwani mteule wa wadi ya Kijini kwa tiketi ya CCM.**

# Dk. Mwinyi aahidi neema kwa wajane

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekutana na Jumuiya ya Wanawake Wajane na kuahidi kuwatambua kwa kuwaingiza katika mfuko wa hifadhi ya jamii.

Pia ameahidi kuwapatia mikopo itakayosaidia kuwakwamua kiuchumi, hatua ambayo itawaletea maendeleo ya kiuchumi.

Akizungumza na wanawake hao jana katika ukumbi wa Sheikh Idris Abduliwakil, Dk. Mwinyi alisema akichaguliwa kuwa rais, anakusudia kuyatambua makundi maalumu ikiwamo watu wenye ulemavu, wazee pamoja na wanawake wajane walioachwa na waume zao na hivyo kuweza kuzitumia fursa mbalimbali za kiuchumi.

Alisema makundi hayo yatapatiwa mikopo isiyo na riba, ambapo serikali itachukua jukumu la kulipa riba katika taasisi za fedha.

**Nawaomba wanawake wajane waitumie jumuiya hii kwa ajili ya kuunganisha nguvu zao na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili ikiwamo kupewa jukumu la malezi ya watoto na wanaume waliowapa talaka.**

"Nazitambua changamoto kubwa zinazowapata wanawake walioachwa na waume zao, hivyo kuishi katika mazingira magumu. Nikichaguliwa nitalichukua suala hilo kwa kuyaingiza makundi maalumu katika mfumo wa kupata mikopo isiyo na riba na kupata fedha kwa ajili ya kufanya miradi midogo na kuondokana na hali ngumu ya maisha," alisema.

Pia alisema anakusudia kuangalia mfumo mzuri wa sheria za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake wakati wanapopewa talaka na kuachiwa mzigo wa familia ikiwamo watoto.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wajane, Tabia Makame, alisema wakati umefika kwa makundi maalumu ya wanawake wakiwamo wajane kutambulia na kuingia katika vyombo vya kutunga sheria, ili sauti zao zisikike kwa ajili ya kuyapatia ufumbuzi matatizo yao.

Alisema wajane wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo kuachiwa mzigo wa familia pamoja na watoto na hivyo kushindwa kumudu majukumu ya kutunza watoto na kuwapatia mahitaji ya msingi ikiwamo elimu na chakula.

"Tunakuomba ukifanikiwa kuingia madarakani sisi wanawake wajane tunahitaji tupatiwe ufumbuzi wa matatizo yetu ikiwamo suala la udhalilishaji wa kijinsia kwa kuachiwa malezi ya watoto wakati hatuna uwezo wa kifedha," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Jumuiya ya Wanawake Wajane ambaye ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema wameanzisha taasisi hiyo kwa ajili ya kuyafikia malengo ya kujikomboa na umaskini kutokana na kukabiliwa na mzigo mkubwa wa maisha.

"Nawaomba wanawake wajane waitumie jumuiya hii kwa ajili ya kuunganisha nguvu zao na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili ikiwamo kupewa jukumu la malezi ya watoto na wanaume waliowapa talaka," alisema.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Mustafa Aboud Jumbe (katikati), akizungumza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Tanzania Bara, Dk. Zainab Chaula, baada ya utiaji saini makubaliano ya huduma za mkongo kati ya ZICTIA na TTCL, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mtoto wa Turky ajitosa kurithi nafasi ya baba yake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTOTO wa aliyekuwa mgombea ubunge wa Jimbo la Mpendae, Salum Turky, ameonyesha nia ya kumrithi baba yake nafasi hiyo kupitia Chama Cha Mapinduzi CCM.

Mtoto huyo, Taufiq Salum Rurky, jana alichukua fomu ya kugombea nafasi hiyo ya ubunge kupitia CCM kutaka kuchukua nafasi ya baba yake huyo, aliyefariki dunia hivi karibuni.

Turkey alichukua fomu katika ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) zilizoko Maisara, Zanzibar, baada ya kushinda katika kura ya maoni na Kamati Kuu ya CCM kumpitisha kugombea nafasi hiyo.

Mgombea huyo anamrithi baba yake ambaye amefariki dunia Septemba 14, mwaka huu, ambapo alikua akitetea nafasi hiyo kwa kipindi kingine baada ya kuliongoza jimbo hilo miaka 10.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu hiyo, Taufiq, alisema endapo atashinda atahakikisha anaendeleza yale yote mazuri aliyoyafanya baba yake jimboni humo ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa jimbo hilo.

Mambo makubwa yamefanywa na baba yake katika kipindi cha uongozi wa miaka 10 ikiwamo maendeleo ya sekta ya elimu na kusaidia makundi mbalimbali ikiwamo miradi ya wanawake ambayo aliahidi kuyaendeleza.

"Nimejipanga kuvaa viatu vilivyoachwa na baba yangu vya uongozi na kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu na wajasiriamali wanawake," alisema.

Mgombea huyo aliongozana na mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, ambaye alisema amekuja kuunga mkono familia ya marehemu Turky ambao ni marafiki wa muda mrefu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja kinauzwa Bunju Beach kwa Moga (Square meter 1373). Kwa mawasiliano piga simu namba **0658 834 004.** Hakuna dalali.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**JARED EDMIN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0753/0035** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BIIRABO SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/64552/2020.**

115912102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**OMARI ALI HASSAN**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili **T 887 AJQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/674103/2020.**

115912802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;273/2020**

**Ombi la ABDULKARIM HALFAN ZANDA.,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HALFAN ATHUMAN ZANDA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/09/2020.

Tarehe 16/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115912502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THE CONGREGATION OF ST.GEMMAGALGANI SISTERS** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 150 AWZ** aina yake TOYOTA HIACE yenye ingine namba **IKZ0136241** na chasis namba **KZH1201001069** na rb namba **/MOR/MOR/RB/13692/2020.**

215912202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA**

**MAOMBI NA. 13/2020**

**SALUM S.A. MPENDA............MLETA MAOMBI**

**VERSUS**

**KILOMBERO FILING STATION............................MJIBU MAOMBI**

**NDANDE A. ABDALLAH.......................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA NDANDE A. ABDALLAH**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilosa, tarehe 24/09/2020 wenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hutahudhuria, maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi. Imesainiwa leo tarehe 16 mwezi 09 mwaka 2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
KILOSA

115913002

## KUPOTEA KWA VYETI



**OCTAVIAN RWEGOSHORA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0397/0069** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RULENGE SEKONDARI mwaka 2005. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0118/0505** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KATOKE SEMINARY mwaka 2008. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOS/RB/10957/15.**

115911902

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MALYETA S. MAHOLA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 790 APK** Chassis namba **L7GPCKLY2D4068725.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/683288/2020.**

115912002

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara wa Nyumba iliyopo Mtaa wa Basihaya (BOKO) - Wilaya ya Kinondoni. Nyumba hii ni mali ya mdaiwa Sugu, **Ndugu Helena Elias Kibiki,** mnada huo utafanyika tarehe 10/10/2020. Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo anaodaiwa. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo Basihaya-Boko. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Kwa mawasiliano fika kwenye ofisi zetu Victoria 5th floor au piga. 0652113262**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;266/2020**

**Ombi la CECILIA ROLAND MZENGA ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ROLAND FRANCIS MZENGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/09/2020.

Tarehe 10/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115911802


**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**

**Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**



Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wanajeshi wanne jela miaka 10

**YAOUNDE,** Cameroon

WANAJESHI wanne wa Cameroon wamehukumiwa kifungo cha miaka 10 jela, kutokana na mauaji ya wanawake wawili na watoto wawili yaliyotekelezwa mwaka 2015.

Mauaji hayo yalinaswa kwenye kanda ya video, ambayo ilisambazwa mitandaoni mwaka 2018 ikionyesha namna wanawake hao walivyofungwa macho na kupigwa risasi.

Awali, serikali ilikana na kusema video hiyo ni taarifa ya kughushi, lakini baadaye ikawakamata wanajeshi saba.

Uchunguzi wa BBC Africa Eye, ambao uliangazia kisa hicho ulionyesha kilichotokea katika kijiji kimoja cha mbali Kaskazini mwa Cameroon.

Pia iliwaonyesha maofisa watatu waliotekeleza kitendo hicho.

Katika video hiyo, maofisa wanaonekana wakiwatuhumu wanawake hao kwa kujihusisha na Boko Haram, kundi la wanamgambo wa Kiislam, ambalo mashambulio yake katika nchi jirani ya Nigeria yamesambaa na kuvuka mpaka.

Wanawake hao ambao, miongoni mwao alikuwamo aliyekuwa amemfunga mtoto mchanga mgongoni, walitembezwa kwenye barabara ya vumbi huku wakifungwa macho kwa kitambaa na kisha kupigwa risasi mara 22.

Saba kati ya wale walioshtakiwa katika mahakama ya kijeshi mji mkuu wa Yaoundé, waliondolewa mashtaka.

Maofisa wanne walihukumiwa kifungo cha miaka kumi jela kwa kutekeleza mauaji ama kushirikiana kufanya uhalifu, huku maofisa wa tano akipokea kifungo cha miaka miwili kwa kurekodi kanda ya video ya tukio hilo na kuisambaza.

Uchunguzi wa BBC ulifanya kisa hicho kuzua gumzo kimataifa huku baadhi ya watu wakieleza masikitiko yao kwenye mtandao wa Twitter. Taarifa hiyo iliwafikia mamilioni ya watazamaji mitandaoni.

Nchi ilipatwa na mshangao wakati video hiyo ilipotolewa mara ya kwanza mwaka 2018 lakini serikali ilipuuzilia mbali.

Awali, Msemaji wa Serikali alisema video hiyo ilirekodiwa nchini Mali na sare za kijeshi zilizoonyeshwa kwenye kanda hiyo, siyo zile zinazotumiwa na wanajeshi wa nchi hiyo katika eneo hilo la Cameroon.

Lakini, ushahidi uliendelea kutolewa hali ambayo ilifanya kuwa vigumu kuficha.

Ni nadra sana kwa wanajeshi kufungwa kwa kuua raia nchini Cameroon, lakini ishawahi kufanyika tena. **BBC**

# Jaji Mkuu wa Kenya ataka Bunge livunjwe

**NAIROBI,** Kenya

JAJI Mkuu Kenya, David Maraga, amemshauri, Rais Uhuru Kenyatta, kulivunja Bunge kwa sababu halina wabunge wanawake wa kutosha.

Katika barua yake kwa Rais Kenyatta, jaji huyo alisema bunge kushindwa kuwa na wabunge wengi wa kike ni ukiukaji wa katiba na ubaguzi dhidi ya wanawake.

Katiba inasema kwamba jinsia moja haiwezi kudhibiti zaidi ya theluthi mbili ya viti vya bunge. Hatahivyo wanawake wana viti vichache ikilinganishwa na viti 116 vinavyohitajika katika bunge hilo la wabunge 350.

"Bunge limefeli ama kupuuza sheria zinazohitajika kuidhinisha sheria hiyo ya jinsia, licha ya maagizo manne ya mahakama. Wacha tuhisi maumivu iwapo ni lazima," alisema Jaji Maraga.

**Hatuwezi kusahau kuhusu changamoto zinazotukabili tunapojaribu kuidhinisha suala hili na kuligeuza bunge kuwa eneo la kupigana kutokana na jinsia.**

Spika wa Bunge, Justin Muturi akijibu hilo alisema kwamba kuvunjwa kwa bunge ni chaguo lisilowezekana. Katiba mpya ya Kenya ilizinduliwa 2010, na sheria ya jinsia kuhusu theluthi mbili ilifaa kuidhinishwa baada ya miaka mitano.

Kukiwa na mjadala huo, bunge hilo lenye wanaume wengi halijapata mbinu ya kupata wanawake wengi bungeni, huku baadhi ya wabunge hao wakihoji dhidi ya kubuni viti vingi hususan vya wanawake na badala yake kuwataka wanawake kuingia katika kinyang'anyiro cha kuwania ubunge mashinani.

"Hatuwezi kusahau kuhusu changamoto zinazotukabili tunapojaribu kuidhinisha suala hili na kuligeuza bunge kuwa eneo la kupigana kutokana na jinsia," alisema katika taarifa yake juzi.

Jaji Maraga alisema kwamba bunge la 10 halikuwa na muda wa kutosha kuidhinisha sheria inayohitajika kuhalalisha sheria hiyo ya jinsia.

Kulingana na Maraga, mahakama ya upeo chini ya aliyekuwa Jaji Mkuu Willy Mutunga, aliagiza bunge kuidhinisha sheria hiyo kufikia Agosti 27, mwaka 2015.

Jaji huyo alisema kwamba pingamizi kadhaa ziliwasilishwa mahakamani zikilitaka bunge kuidhinisha sheria hiyo.

"Hata hivyo Bunge lilishindwa kuidhinisha miswada iliyowasilishwa mbele yake".

Maraga alisema sheria hiyo ya jinsia inazuia aina yoyote ya ubaguzi katika uteuzi na uchaguzi nchini kulingana na jinsia.

"Wanawake na wanaume wana haki ya fursa sawa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii." **BBC**



Mwanamke mjamzito anayedaiwa kukatwa tumbo na mume wake na kujifungua mtoto akiwa amefariki akipatiwa huduma ya kwanza. **PICHA: CHITRANJAN SINGH/BBC**

# Ajifungua mtoto mfu kwa kipigo cha mume

**NEW DELHI,** India

POLISI nchini India imesema mjamzito ambaye anadaiwa kujeruhiwa kwa upanga na mume wake, amejifungua mtoto mfu wa kiume.

Familia ya mwanamke huyo inadai kuwa mwanaume huyo alimshambulia akitaka kujua jinsia ya mtoto.

Walisema wanandoa hao wana watoto watano wa kike na kwamba mwanaume huyo amekuwa akimhangaisha mke wake amzalie mtoto wa kiume.

Mwanaume huyo ambaye tayari amekamatwa, amekanusha madai ya kumshambulia makusudi mke wake akisema ilikuwa ni ajali.

Kisa hicho kilitokea katika Wilaya ya Badaun, Uttar Pradesh, Jimbo la India lililo na watu wengi zaidi Kaskazini mwa nchi.

Maofisa wameiambia BBC kwamba, mwanamke aliyejeruhiwa anaendelea kupokea matibabu na kwamba hali yake imeimarika katika hospitali ya mji mkuu wa Delhi.

Kwa mujibu wa ndugu yake, mwanamke huyo alipelekwa Delhi siku ya Jumapili, baada ya ushauri wa daktari kwa sababu hali yake ilikuwa mbaya.

Mume wake aliviambia vyombo vya habari kuwa alimrushia upanga, lakini hakujua utamuumiza vibaya.

"Nina watoto watano wa kike, mwanangu mmoja wa kiume amefariki. Najua watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu. Sasa chochote kitakachotokea, kitatokea."

Kila mwaka, watoto wa kike karibu 460,000 wanauawa kupitia utoaji mimba huku vifo vingi vya watoto wa kike wanaozaliwa na kutelekezwa baada ya kuzaliwa vikiripotiwa.

Mwaka 2018 ripoti ya serikali ya India ilisema hamu ya kutaka watoto wa kiume imechangia kuzaliwa kwa watoto wa kike milioni 21, ambao 'hawapatikani'.

Ripoti hiyo ya Wizara ya Fedha ilibaini kuwa wanandoa wengi wanaendelea kuzaa hadi wapate mtoto wa kiume. **BBC**

# ARSENAL YAMSAJILI KIPA RUNARSSON



**LONDON,** England

ARSENAL imethibitisha kumsajili golikipa, Alex Runarsson kutoka timu ya Dijon ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni moja.

'Washikabunduki' hao walimpoteza kipa wao, Emiliano Martinez ambaye alijiunga na Aston Villa wiki iliyopita.

Martinez alionyesha kiwango cha kuvutia katika nusu ya pili ya msimu uliopita na kuisaidia Arsenal kushinda Kombe la FA na Ngao ya Jamii, lakini aliondoka na kwenda Villa Park kutafuta nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza.

Huku Bernd Leno akiwa ndiye chaguo la kwanza, Runarsson mwenye umri wa miaka 25, ametua hapo kwa ajili ya kuwa msaidizi wake.

"Tunataka kutengeneza ushindani wa kiafya na tunatarajia Alex atafanya hivyo katika nafasi ya kipa," alisema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.

Runarsson ambaye ni golikipa wa kimataifa wa Iceland, atavaa jezi namba 13.

# Guardiola: Hakuna kama De Bruyne



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesifia kiwango cha Kevin De Bruyne wakati akiiongoza Manchester City iliyowakosa wachezaji wake wengi kutokana na majeraha na kuiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Wolves, Jumatatu.

Guardiola alielekea kwenye Uwanja wa Molineux, huku wachezaji wake saba wakikosekana kutokana na kuwa majeruhi, lakini Man City iliweza kulipiza kisasi kwani msimu uliopita ilifungwa mara mbili na Wolves.

De Bruyne alikuwa nyota wa City, akifunga kwa penalti dakika ya 20 kabla ya kuhusika kwenye mabao mawili ya Phil Foden na Gabriel Jesus.

"Tangu turiporudi baada ya mechi za kimataifa, kila wakati kwenye mazoezi alionyesha majukumu yake," alisema Guardiola, ambaye alishuhuhudia timu yake ikifungwa bao la kufutia macho na Raul Jimenez dakika ya 78, akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa sasa ni mchezaji muhimu sana kwetu sisi. Mara zote alikuwa hivyo, lakini kwa hali ilivyo sasa ni mchezaji muhimu sana kwetu.

"Alifunga penalti kwa ustadi, alifunga wakati muhimu. Halafu alitoa pasi za mwisho. Alicheza vizuri sana, kama ilivyo kwa timu nzima.

"Anapenda kucheza soka, hana presha na yupo kwenye kiwango bora zaidi kwa sasa."

# Silva: Nimekuja Chelsea kushinda ubingwa EPL

**LONDON,** England

THIAGO Silva amesema amejiunga na Chelsea lengo lake likiwa ni kushinda taji la Ligi Kuu ya England, na si tu kupata uzoefu wa kucheza soka la Uingereza.

Mlinzi huyo wa kati, ambaye jana Jumanne alitimiza umri wa miaka 36, alisaini mkataba wa mwaka mmoja wenye kipengele cha kumwongeza miezi 12 baada ya kuondoka Paris Saint-Germain.

Silva amesema malengo yake makubwa ni kuisaidia Chelsea kushinda taji la Ligi Kuu pamoja na kuendelea kulizoea soka la Uingereza.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil anaamini kwa kufanya vizuri na Chelsea kutamwezesha kucheza michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka 2022.

"Kwa namna ninavyoona, ni ligi ngumu zaidi duniani, huku kukiwa na timu sita au saba zinazopigania taji la Ligi Kuu," alisema Silva, ambaye ametumia miaka nane akicheza kule PSG na mchezo wake wa mwisho ukiwa ni fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiiambia tovuti ya Chelsea.

"Matarajio yangu ni kucheza kila siku na nina njaa ya kushinda. Kushinda kila kitu kilichopo mbele yangu. "Kuja kwenye Ligi Kuu ya England, malengo yangu makubwa ni kushinda taji na nina uhakika kwamba tunaweza kulipigania taji hilo."



HABARI MICHEZO

# Pioli akunwa kiwango cha Ibrahimovic AC Milan

**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa AC Milan, Stefano Pioli, amemsifia Zlatan Ibrahimovic kwa kufunga mabao mawili dhidi ya Bologna na kusema amethibitisha yeye ni bingwa.

Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, alifunga mara mbili wakati Milan ikianza msimu mpya wa Serie A kwa ushindi wa 2-0 pale katika dimba la San Siro, ambako nyota wa Bologna, Mitchell Dijks alitolewa nje kwa kadi nyekundu, kwenye mchezo wa juzi Jumatatu.


Pioli alipaza sauti kumsifia straika huyo, lakini akasema Ibrahimovic angeweza kung'ara zaidi kama Milan wangekuwa bora zaidi.

"Wakati timu inafanya kazi, mbinu za mchezaji binafsi ni muhimu, halafu Zlatan ni bingwa na anathibitisha kila wakati," alisema kocha huyo Mkuu wa Milan akiiambia Sky Sport.

"Timu inajiamini, anajua namba ya kucheza hata kwenye mazingira magumu. Anajua kujitolea yeye mwenyewe.

"Halafu kuna ubora wa ubunifu kwa mchezaji na nina furaha kwamba tumeanza ligi vizuri."

Milan ilimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo msimu uliopita na sasa inajiandaa kucheza na Klabu ya Bodo kutoka nchini Norway kuwania kufuzu mashindano ya Ligi ya Europa, Alhamisi.







# MORATA AKARIBISHWA JUVENTUS

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imemkaribisha Alvaro Morata pale Turin wakati mshambuliaji huyo akitarajiwa kurudi kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Morata ameripotiwa anajiandaa kujiunga na Juve kwa mkopo kutoka Atletico Madrid katika dili linalotajwa kuwa na thamani ya euro milioni tisa na klabu hiyo ikiwekewa kipengele cha kumnunua nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, kwa euro milioni 45.

Juventus, ambayo imekuwa ikitafuta mshambuliaji, imemkaribisha Morata kurudi Turin.

"Alvaro Morata anarudi mjini," Twitter ya klabu hiyo ilisomeka huku ikiwekwa picha ya mshambuliaji huyo.

Morata anatarajia kurudi katika kipindi cha pili kule Juve, ambako alifunga mabao 27 katika mechi 93 alizocheza kwa misimu miwili aliyokaa kati ya mwaka 2014 na 2016.

Akarudi Real Madrid kwa msimu mmoja kabla ya kujiunga na Chelsea na baadaye Atletico, ambako alifunga mabao 12 kwenye LaLiga katika mechi 34 msimu uliopita.

Huku Gonzalo Higuain akiwa ameondoka kwenda kujiunga na Inter Miami, Juve imekuwa ikitafuta mshambuliaji wa kati, huku ikihusishwa na majina kama Luis Suarez wa Barcelona na straika wa AS Roma, Edin Dzeko.

# *Lampard kumkalia kitako Kepa*

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesema atajitahidi kurudisha makali ya mlinda mlango wake, Kepa Arrizabalaga baada ya kufanya makosa yaliyosababisha kufungwa na Liverpool kwenye Ligi Kuu England, Jumamosi.

Chelsea ilikutana na kipigo cha 2-0 kutoka kwa Liverpool katika mchezo wa Ligi Kuu England raundi ya pili, huku Kepa ambaye alikuwa analaumiwa kutokana na makosa, pia akifanya kosa lililosababisha bao la pili la Sadio Mane.

Kipa huyo pia alifanya kosa katika mchezo wa ufunguzi wa pazia la EPL dhidi ya Brighton.

Makosa hayo yameifanya Chelsea kuanza kutafuta mbadala wa Kepa ambaye amekuwa na makosa ya hapa na pale, na jina la mlinda mlango wa Rennes, Edouard Mendy linatajwa kuwamo The Blues msimu huu.

"Ni kweli ni makosa ya wazi ambayo yamekuwa yakitugharimu," alisema Lampard akizungumzia mapungufu ya kipa huyo raia wa Hispania.

"Tunatakiwa kuendelea kupambana, Kepa anatakiwa kuendelea kujifunza huku akipewa msaada wa karibu na si kumshambulia.

"Binafsi wachezaji wanahitaji msaada mkubwa ili kuanza kupata nguvu ya kufanya vizuri, nimekuwa karibu kwa kila mchezaji ili anieleze shida yake ili nijue nafanyaje."

Kepa mwenye umri wa miaka 25, anaendelea kushikilia rekodi ya kuwa mlinda mlango ghali zaidi kutokana na kununuliwa kwa pauni milioni 71 akitokea Athletic Bilbao miaka miwili iliyopita.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVER YAONGOZA MBIO KUMWANIA MBAPPE

●●● Bado haijajulikana nani atakuwa mshindi katika mbio kati ya Liverpool na Madrid, lakini...

**LIVERPOOL,** England

WAKATI uvumi ukibainisha kwamba, Real Madrid ndiyo yenye nafasi kubwa zaidi kumtwaa nyota wa Ufaransa, Kylian Mbappe, Liverpool kwa sasa inaongoza kwenye mbio hizo.

**Kwa mujibu wa gazeti la L'Equipe vijogoo hao wa Anfield ndio wapo kwenye nafasi nzuri kuipata nafasi ya mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain.**

Mbappe mwenye umri wa miaka 21, mkataba wake wa sasa na PSG unamalizika mwaka 2022, huku majaliwa yake yakiwa yanapamba zaidi vyombo vya habari kwa sasa.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, inaonekana kwamba huu unaweza kuwa msimu wake wa mwisho kucheza pale PSG.

Majaliwa ya Mbappe yataamuliwa mwakani kama mshambuliaji huyo atabaki PSG au kwenda Real Madrid ama Liverpool.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ameripotiwa kwamba anamtaka mchezaji huyo kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake.

Pia Mbappe mwenyewe ameripotiwa kuwa shabiki mkubwa wa Liverpool na amejiunga nao kwenye mitandao yake yote ya kijamii.

Hata hivyo, Mfaransa mwenzake, Zinedine Zidane ambaye ni kocha mkuu wa Madrid inaaminika kwamba ni shabiki wake mkubwa na hajawahi kuficha hisia zake za kutaka kufanya kazi na Mbappe.

Ripoti zaidi zinasema kwamba, Zidane amekuwa akiwasiliana mara kwa mara na Mbappe akijaribu kumshawishi ajiunge na Madrid.

Hata hivyo, bado haijajulikani nani atakuwa mshindi katika mbio hizo za kumwania Mbappe kati ya Liverpool na Madrid.

## ZISIKUPITE

### UNITED NIA KWA UPAMECANO



KLABU ya Manchester United inania pia ya kumsajili mlinzi wa RB Leipzig na Ufaransa, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 21. ***(Telegraph)***

### MADRID YAMPOTEZEA DELE

REAL Madrid haina mpango wa kumsajili kiungo wa England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, kutoka Tottenham. ***(Talksport)***

### CRYSTAL YAMKANA BREWSTER




KLABU ya Crystal Palace imekana kutoa ofa ya pauni milioni 25 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji kinda wa Liverpool na timu ya Taifa ya Vijana ya England chini ya miaka 21, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 20. ***(Goal)***

### EVERTON KUMSAJILI ARIAS

EVERTON ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Atletico Madrid na Colombia, Santiago Arias mwenye umri wa miaka 28. ***(Liverpool Echo)***

### TELLES MATUMAINI KWA UTD



MLINZI wa kushoto wa Porto, Alex Telles ana matumaini ya kukamilisha uhamisho wa kwenda Manchester United, ingawa klabu hizo hazijafikia makubaliano ya ada ya uhamisho kwa ajili ya Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Guardian)***

### SEILLA KUTOMUUZA KOUNDE

KLABU ya Sevilla imethibitisha kwamba imekataa ofa kwa ajili ya mlinzi wake, Jules Kounde. Mfaransa huyo ambaye anaichezea timu ya taifa ya vijana chini ya umri wa miaka miaka 21, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Manchester City. ***(Goal)***

### DUNCAN KUTUA DERBY




MSHAMBULIAJI wa zamani wa timu ya vijana ya Liverpool, Bobby Duncan mwenye umri wa miaka 19, anajiandaa kuondoka Fiorentina na kwenda kujiunga na Derby County. ***(The Athletic)***

### MORATA HUYO JUVENTUS

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kurejea Juventus kutoka Atletico Madrid. ***(Goal)***

### SUARES KUTUA ATLETICO



LUIS Suarez mwenye umri wa miaka 33, amekubali kuvunja mkataba wake na Barcelona ili kujiunga na Atletico Madrid. ***(RMC - via Mail)***

### AURIER AWANIWA SPARTAK

KLABU ya Spartak Moscow inamtaka beki wa kulia wa Tottenham na Ivory Coast, Serge Aurier mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports - via Boot Room)***

### TORINO YAMWACHA TORREIRA



TORINO imeondoa nia yake ya kutaka kumsajili kiungo wa Arsenal na Uruguay, Lucas Torreira, lakini Atletico Madrid ipo kwenye mbio za kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## KMC: Kila mechi ni vita msimu huu

**Na Adam Nyangasa,** TUDARCo

HUKU wakiendelea kutesa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kushinda mechi zake tatu za awali, Kaimu Kocha Mkuu wa KMC FC, Habibu Kondo, amesema mikakati yake ni kuendelea kupambana hadi mwisho kutafuta alama muhimu katika kila mechi iliyopo mbele.

KMC ambayo msimu uliopita ilimaliza katika nafasi ya 13 ikiwa na alama 46, pointi moja zaidi ya timu zilizocheza mechi ya mchujo kuwania kujinusuru kushuka daraja, imeanza vema msimu huu huku pia ikiwa timu inayoongoza kwa kucheza na nyavu hadi sasa baada ya kufunga mabao nane na kuruhusu nyavu zake kutikiswa mara mbili tu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kondo alisema hataki kuona makosa ya msimu uliopita yanajirudia, hivyo anapambana kuhakikisha wachezaji wake wanapata matokeo chanya katika kila mechi iliyopo mbele yao.

Alisema kikosi chao kipo 'fiti' na baada ya kuibuka na alama tatu dhidi ya Mwandui FC, sasa wanaelekea Bukoba kutafuta pointi nyingine dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa keshokutwa, Ijumaa.

"Msimu huu ligi inaushindani mkubwa, nimejipanga kutafuta alama muhimu katika mechi zangu zote iwe nyumbani au ugenini, ili kuhakikisha tunapata matokeo chanya na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo," alisema Kondo.

## Mkwasa kugeukia safu ushambuliaji

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu Klabu ya Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, amesema licha ya kupata pointi tatu katika mchezo uliopita, baada ya kuifunga Gwambina FC kwa bao 1-0, safu yake ya ushambuliaji bado ina mapungufu makubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa na kuwapongeza wachezaji wake kwa kazi kubwa waliyoifanya mpaka kupata matokeo hayo wakiwa nyumbani.

"Mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, lakini tunashukuru tumepata pointi tatu tukiwa nyumbani, kwa upande wetu ushindi huo ni muhimu kwani tunapata nguvu ya kujipanga na michezo ijayo kuhakikisha tunashika nafasi nzuri," alisema Mkwasa.

Aidha, alisema mapungufu ya safu ya ushambuliaji ambayo ameyabaini, ataendelea kuyafanyia kazi, ili yasijitokeze tena kwenye mchezo wao ujao watakapoikaribisha Biashara United Septemba 27, mwaka huu katika uwanja huo.

Alisema kwa sasa wanaelekeza nguvu zote katika mchezo huo na na kwamba anaiheshimu Biashara United kutokana na kuwa miongoni mwa timu nzuri, ambayo katika michezo yake ya mwanzo imeanza vizuri.

Hadi sasa Ruvu Shooting imejikusanyia pointi nne ikiwa nafasi ya 10 baada ya kushinda mechi moja, sare moja na kupoteza mchezo mmoja katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu.

# MTIBWA YAIONYA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zubery Katwila, amesema amejipanga vizuri kukisuka kikosi chake kwa kukipa mbinu hususani mabeki kuweza kukabiliana na washambuliaji wa Yanga, watakapokutana katika mechi ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema amewashuhudia Yanga wakiwa wanacheza na Kagera Sugar na kuona mapungufu na ubora wa wapinzani wao hao, hivyo anaendelea kuwapa mbinu wachezaji wake hasa mabeki kuwa makini na safu ya ushambuliaji ya Yanga inayoongozwa na Mghana Michael Sarpong.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wachezaji wake wanapambana kutafuta alama muhimu katika kila mechi wanayocheza wakiwamo kutafuta matokeo mazuri katika michezo yao ya nyumbani.

**"Katika mechi tatu tulizocheza, nimevuna alama mbili nyumbani dhidi ya Ruvu Shooting na Simba na nimekuja kupata alama tatu ugenini nilipocheza na Ihefu, sasa tunajipanga dhidi ya Yanga kuhakikisha haitoki Jamhuri.**

"Nawaheshimu sana Yanga imefanya usajili mzuri, nimewashuhudia na kufanyia kazi mapungufu na ubora wao, ninachowaambia wasije Morogoro wakiwa na matokeo yao kwa sababu malengo yetu ni kupata alama muhimu katika kila mechi iliyopo mbele yetu hasa uwanja wa nyumbani," alisema Katwila.

Alisema Simba walienda na matokeo yao na waliondoka na alama moja, hivyo akaionya Yanga isiende na matokeo yao kwani inaweza kukutana na balaa la kuondoka mikono mitupu.

Katwila alisema, wanahitaji kuhakikisha wanapambana kusaka alama muhimu kwa kila mechi, mzunguko huu wa kwanza na kutohitaji kurudia makosa ya msimu uliopita kumaliza ligi kwa presha kubwa ya kunusurika kushuka daraja.

Baada ya kurejea na alama tatu kutoka Mbeya dhidi ya Ihefu FC, Mtibwa yenye pointi tano katika nafasi ya saba ya msimamo wa ligi hiyo, Jumapili inatarajia kuikaribisha Yanga katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.




Rais wa Klabu ya Al Ahly ya Misri, Mahmoud El Khatib akimkabidhi Ofisa Mtendaji wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez (kulia), jezi ya timu hiyo baada ya wiki hii kufanya ziara ya kiuhusiano na kujifunza mambo mbalimbali ya kibiashara akiwa na mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mulamu Nghambi (kushoto). Klabu hizo zimekubaliana kucheza mechi ya kirafiki hapa nchini. **PICHA: SIMBA**

## *Mwanadada mwingine ashinda mil. 267/- Jackport ya SportPesa*

**Na Mwandishi Wetu**

KITITA cha Sh. 267,800,060 cha Jackpot ya SportPesa kimemwangukia mwanadada Lilian Ngitoria Laizer wa Turiani, Morogoro baada ya kubashiri kwa usahihi matokeo ya mechi zote 13.

Ngitoria, 28, ambaye ni mjasiriamali, anakuwa mwanamke wa pili kushinda Jackpot ya SportPesa baada ya Scolastika Ngwalueson ambaye alishinda shilingi 260,319,960 Septemba mwaka jana, naye akibashiri kwa usahihi mechi zote13.

Akimtangaza mshindi huyo wa awamu ya tano, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alianza kwa kumpongeza Laizer kwa ushindi huo wa shilingi milioni 267.8 alioupata kwa kucheza na kushinda Jackpot.

"Tunaendelea kuwa wabunifu zaidi, lengo kuu likiwa kama kampuni kubadilisha ama kuboresha maisha ya Watanzania kupitia michezo mbalimbali hasa mpira wa miguu.

"Napenda kumtangaza rasmi Lilian Laizer kuwa ndiye mshindi wa Jackpot yetu ya wiki iliyopita. Fedha hizi alizoshinda tayari zipo kwenye akaunti yake ya SportPesa na tunafuata utaratibu, ili kuhakikisha tunamkabidhi maana malipo yetu sisi ni papo hapo mara baada ya kuibuka mshindi," alisema Tarimba.

SportPesa ni kampuni inayozidhamini klabu kubwa hapa nchini za Simba, Yanga na Namungo FC ambayo ilianza udhamini wake mwaka 2017 tangu ilipoanza kuchezesha michezo ya kubashiri hapa nchini.

## Azam yaivulia kofia Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kushinda bao 1-0 dhidi ya Mbeya City, Azam FC imesema kuwa ilipata wakati mgumu kupata ushindi huo kutokana na wenyeji wao kucheza kwa juhudi kubwa, na kutumia nguvu nyingi na kupambana pia.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, amesema timu yao ilibidi ipigane na kutoa jasho na machozi kupata ushindi huo kutokana na kukutana na timu iliyokuwa na wachezaji wapambanaji, wanaojituma na kutumia nguvu.

Lilikuwa ni bao pekee la Mnyarwanda Ally Niyonzima lilitosha kuipa ushindi timu hiyo ambayo mpaka sasa inashika nafasi ya pili kwa pointi tisa, nyuma ya KMC ambayo inaongoza ligi kwa tofauti ya magoli.

Michezo
Jumatano Septemba 23, 2020
Nipashe



Liver yaongoza mbio kumwania Mbappe UKURASA 22

MILIKI...



Washambuliaji wa Simba, Chris Mugalu na Miraji Athumani, wakiwania kumiliki mpira dhidi ya beki wa African Lyon, katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam jana. Simba ilishinda 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yaileta Al Ahly kukipiga kwa Mkapa

## ●●● Barbara awavuta kuja kuwajengea kituo cha kukuza vipaji nchini, waichapa Lyon 2-0...

**Na Saada Akida**

ZIARA ya kimafunzo ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez sambamba na mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mulamu Nghambi katika Klabu ya Al Ahly ya Misri, imezaa matunda baada ya klabu hizo mbili kukubaliana mambo kadhaa ya kimaendeleo, ikiwa ni pamoja ya kucheza mechi ya kirafiki hapa nchini, imeelezwa.

**Viongozi hao wa Simba waliondoka nchini mapema wiki hiii kuelekea Misri kwa ajili ya kufanya ziara ya kujenga ushirikiano kwa klabu hizo mbili, ikiwa na malengo ya kupata uzoefu juu ya uendeshaji wa soka kisasa.**

Katika ziara hiyo, ujumbe huo wa Simba ulikutana na Rais wa Klabu ya Al Ahly, Mahmoud El Khatib, na kukubaliana mambo kadhaa ya kimaendeleo ambayo yataifaidisha nchi kisoka na Klabu ya Simba.

Katika ziara hiyo, uongozi wa Simba umesema moja kati ya mambo waliyokubaliana ni mpango wa kucheza mchezo wa kirafiki na Klabu ya Al Ahly ya nchini Misri kwa siku za hivi karibuni, ili kuongeza uhusiano mzuri zaidi kwenye masuala ya michezo.

Aidha, pia umesema wamekubaliana kushirikiana kwenye maeneo ya biashara, ufundi na uendelezaji wa wachezaji kwa kujenga kituo cha kukuza vipaji kwa ushirikiano na timu ya Al Ahly ikiwa ni kituo cha kwanza nje ya Misri (barani Afrika) ambacho kitaendeshwa na Simba na klabu hiyo.

Akizungumzia ziara hiyo, El Khatib alisema lengo kubwa la viongozi wa Simba ni kutaka ushikiriano na kujifunza mambo mbalimbali na kupata uzoefu wa kuendesha klabu hiyo katika mfumo wa kisasa.

"Tunaikaribisha Simba katika ushirikiano wetu, hasa kwa wajumbe hao kuja kujifunza na kupata faida katika uzoefu wa kuendesha klabu yao kuanzia katika uwanja wa michezo, biashara pamoja na mambo ya habari jinsi ambavyo tunafanya hapa kwetu," alisema El Khatib.

Barbara alisema kazi yake kubwa ni kuhakikisha Simba inafanikiwa na kufikia malengo, ikiwamo kupata ujuzi na kushirikiana na klabu kubwa zilizoendelea Afrika.

"Kama nilivyosema mara ya kwanza nilipotambulishwa kuchukuwa nafasi hii, kwanza sitakuwa muongeaji sana bali nitakuwa mtendaji, tunahitaji kuona Simba inafahamika na kuwa na maendeleo kama ilivyo kwa klabu zilizoendelea Afrika," alisema Barbara.

Barbara na Mulamu walitembezwa na kushuhudia viwanja vya kisasa pamoja na sehemu zote za kibiashara ambazo zinamilikiwa na Klabu ya Al Ahly.

Ziara hiyo ya Simba ni mfululizo wa kutaka kujifunza mambo mbalimbali na kuitambulisha klabu hiyo katika ngazi za juu kwani tayari Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohammed 'Mo' Dewji, aliwahi kukutana na Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmed Ahmed, na kisha Rais wa Fifa, Gianni Infantino na wote akiwakabidhi jezi za timu hiyo.

**Katika hatua nyingine**, mabao ya Chris Mugalu dakika ya 47 na Charles Ilamfya dakika ya 53 jana yaliipa Simba ushindi wa 2-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya African Lyon iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

# Yanga yageukia pointi za Mtibwa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Yanga, Mserbia Zlatko Krmpotic (pichani), amesema anaendelea kuwapa wachezaji wake mazoezi magumu ili kuwaweka sawa kuvuna pointi tatu watakapokutana na Mtibwa Sugar Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema lengo lao ni kupata pointi tatu katika mchezo huo ambao watacheza ugenini, huku akiwataka mashabiki wao kuendelea kuipa timu ushirikiano.

Alisema anaamini kila kitu kitakwenda sawa katika mchezo huo na muunganiko wa wachezaji utazidi kupatikana kadri wanavyocheza mechi.

"Natambua ligi ni ngumu na tutajitahidi kupata tena pointi tatu katika mchezo huo baada ya kushinda mechi ya kwanza ugenini dhidi ya Kagera Sugar," alisema.



Kwa upande wa uongozi wa klabu hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema katika mchezo huo mikakati yao ni kuendelea kutoa kila aina ya sapoti kwa wachezaji na benchi la ufundi ili waweze kuwapa burudani mashabiki wao kwa kupata ushindi licha ya mchezo huo kutarajiwa kuwa mgumu na ushindani mkubwa.

"Msimu huu tutahakikisha tunashinda michezo yote na kutwaa ubingwa kwa sababu tumefanya usajili mzuri wa wachezaji ambao tunaamini wataleta ushindani mkubwa katika timu yetu ya Yanga hatuna muda wa kuupoteza," alisema.

Hadi sasa Yanga ina pointi saba baada ya kushinda mechi mbili na kutoka sare moja wakati huu ikiwa katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >